# MAKBETH



William Shakespeare

Mfasiri: S. S. Mushi

TANZANIA PUBLISHING HOUSE

# MAKBETH

William Shakespeare

*Mfasiri*

S. S. MUSHI

TANZANIA PUBLISHING HOUSE LTD
DAR ES SALAAM
1968

TANZANIA PUBLISHING HOUSE LTD
P.O. Box 2138, Dar es Salaam
1968

*Copyright* © S. S. MUSHI

Printed by Tanzania Litho Ltd. P.O. Box 200
Arusha Tanzania

# UTANGULIZI

*Macbeth* ni kitabu kimojawapo cha michezo ya kuigiza ya William Shakespeare ambacho kimependwa na kusifiwa na wengi. Mimi pia nakipenda, hasa kwa sababu ya utamu wa utungo wake wa kishairi, ufasaha wa lugha na mawazo ya Shakespeare yaliyodhihirishwa humo; na zaidi ya vyote, kwa kuwa matatizo na mikasa ya Makbeth, Bibi Makbeth, na wengineo, ni matatizo na mikasa ya kawaida ulimwenguni—kwenye mazingira yo yote na wakati wo wote wanapotokea watu wenye tabia na nia kama zao.

Nilitafsiri kitabu hiki nikiamini kwamba wenzangu wanaopenda michezo ya kuigiza, mashairi kwa jumla, na lugha ya Kiswahili, watapendezwa zaidi na mchezo huu kama wakiusoma kwa lugha ya Kiswahili. Nasema hivyo kwa sababu mchezo huu, kama alivyouandika Shakespeare, haueleweki kwa watu wengi. Lakini sina shaka wengi wataielewa tafsiri yangu.

Shakespeare ameziandika sehemu nyingi za mchezo huu kwa mashairi ya guni. Mizani aliyotumia ni ile iitwayo 'Iambic Pentameter'. Mimi nimezitafsiri sehemu hizo kwa mashairi ya guni, nikitumia mizani ya 16.

Kwa mfano:

MALKOM: Utafanya nini? Kamwe tusitangamane nao:
Kuonyesha huzuni ya uongo ni jambo rahisi
Kwa mtu wa hila. Nitakimbilia Uingereza.

DONALBEN: Nami Ayalendi; tukienda pande tofauti,
Tutaongeza uwezekano wa kusalimika:
Hapa vicheko vya watu vinazisetiri sime:
Na kikulacho ki nguoni mwako.

Lakini, sehemu nyingine, Shakespeare alibadili mizani. Katika sehemu kama hizo, kama msomaji atakavyoona, mimi pia nimebadili mizani. Katika kuandika michezo ya kuigiza, mabadiliko ya mizani ni jambo la lazima kabisa, kwa sababu tunataka kuonyesha mabadiliko katika mawazo na tabia ya moyo wa mchezaji, nyakati tofauti na kwenye hali tofauti. Hapa ndipo inapokuja tofauti kubwa kati ya beti za mashairi ya kawaida na zile za michezo ya kuigiza.

Jambo jingine ni kwamba Shakespeare amewafanya wale Wachawi watatu wazungumze kwa mizani tofauti kabisa; na pia ametumia namna ya vina vinavyoitwa 'Rhyming Couplets'. Mimi, katika kutafsiri sehemu zao, nimetumia mizani ya 12 badala ya 16; na pia nimetumia 'Jozi za Vina'—yaani, kila mistari miwili inayofuatana ikawa na tamko lile lile mwishoni·

Kwa mfano:

MCHAWI 3: Nami nitakupa upepo mwingine.

MCHAWI 2: Nazimiliki hizo nyingine zote,
Na zinakovuma bandarini kote,
Pande zake zote, pia na majira,
Kama ionekanavyo kwenye dira.
Nitamkamua ukoka mkavu:
Usiku na mchana macho makavu,
Na kope zake za hanamu si hoja,
Hatalala usingizi lepe moja n.k.

Tena, Shakespeare mwenyewe hakuwafanya wachezaji wote waseme kwa msemo wa mizani. Nimezitafsiri sehemu kama hizo kwa msemo wa kawaida.

Sina budi kuwaonya wasomaji wote wa tafsiri hii ya kwamba hii si tafsiri ya neno kwa neno, au sentensi kwa sentensi. Kwa hiyo, ni kazi bure kulinganisha kila neno na kila sentensi ya mchezo huu kama alivyouandika Shakespeare mwenyewe na maneno au sentensi katika tafsiri yangu!

Katika onyo hili napenda kuwakumbusha wasomaji mambo matatu. Jambo la kwanza mizani niliyotumia katika kutafsiri mchezo huu siyo lazima ilingane na mizani aliyotumia Shakespeare alipouandika mchezo huu. Pili, mara nyingi katika sentensi hamna ulinganifu kati ya mpango wa maneno ya Kiswahili na mpango wa maneno ya Kiingereza. Tatu, nia yangu ilikuwa kutafsiri "maana" au "habari" wala siyo maneno matupu, kwa kuwa naamini kwamba tafsiri ya kufuatisha neno kwa neno, aghalabu, huwa tafsiri mbaya na isiyoelea. Kwa mfano, utatafsirije sentensi kama hii:

*The near in blood, the nearer bloody?*

Ukifuatisha neno baada ya neno hutapata maana yo yote. Lakini tukitulia na kuchunguza bahari kubwa ya methali za

Kiswahili, tutaona kwamba tunaweza kuitafsiri kwa kutumia methali ya kawaida kabisa ya Kiswahili, kwa mfano:

*Kikulacho ki nguoni mwako. n.k.*

Kuna sehemu nyingi ambazo, kama msomaji atakavyoona, nimezitafsiri kwa kutumia methali za kawaida za Kiswahili, badala ya kufuatisha neno kwa neno.

Kabla ya kuukomesha utangulizi huu, napenda kuwashukuru, bila ya kuwataja majina, marafiki zangu wote ambao wamenitia moyo niikamilishe kazi hii. Nitafanya kosa kama sikumtaja S. M. Kombo, ambaye alikubali kuisoma kazi hii kwa uangalifu na kunipa msaada mkubwa sana. Lakini hivyo siyo kusema kwamba wafadhili hao walaumiwe kwa makosa na upungufu utakaoonekana katika tafsiri hii! Lawama ni yangu mwenyewe. Na ikiwa upungufu wa tafsiri yangu utaudhi baadhi ya wasomaji wangu kiasi cha kuamsha cheche za shauku ya kutoa tafsiri nzuri zaidi ya mchezo huu, hakika hakuna atakayefurahi kunizidi.

SAMUEL STEPHEN MUSHI,
SHIRI—MACHAME, MOSHI,
JAMHURI YA TANZANIA.

## MAJINA YA WACHEZAJI

DANKAN, Mfalme wa Skotia

| | |
|---|---|
| MALKOM<br>DONALBEN | Wana wa Dankan |
| MAKBETH<br>BANKO<br>MAKDAFF<br>LENOKSI<br>ROSS<br>MENTETH<br>ANGASI<br>KATHNE | Majemadari wakuu wa jeshi la Mfalme<br><br>Makabaila wa Skotia |

FLANSI, Mwana wa Banko

SIWADI, Sharifu wa Nothambalendi, jemadari wa majeshi ya Kiingereza

SIWADI MDOGO, Mwanawe

SEYTON, Afisa anayemhudumu Makbeth

MTOTO, Mwana wa Makdaff

Daktari Mwingereza

Daktari Mskotia

SAJINI, Askari msimamizi

BAWABU, Mngoja mlangoni

SHAIBU, Mwanamume mzee

Bibi Makbeth

Bibi Makdaff

Mwanamke mwungwana anayemhudumu Bi. Makbeth

HEKATE, mungu wa kike wa jahanamu

Wachawi watatu wa kike wanaomhudumia Hekate

Waheshimiwa, Watu waungwana, Maafisa, Askari, Wauaji, Wahudumu na Wajumbe

Kivuli cha Banko na Mizuka mingineyo

JANIBU: Skotia na Uingereza

# MAKBETH

## KITENDO CHA I

### Onyesho 1 Nyikani

*Ngurumo na umeme. Wanaingia WACHAWI watatu.*

MCHAWI 1: Sisi watatu tena twonane lini,
Kwenye radi, umeme au mvuani?
MCHAWI 2: Itakapokoma vita na ghasia,
Na mshindi na mshindwa kutokea.
MCHAWI 3: Hayo ni kabla ya jua kuchwa.
MCHAWI 1: Iwe wapi hasa?
MCHAWI 2: Nyikani.
MCHAWI 3: Na huko tuonane na Makbeth.
MCHAWI 1: Nakuja, ewe paka kijivujivu.
MCHAWI 2: Chura anaita.
MCHAWI 3: Naja sasa hivi.
WOTE: Wema kwa wengine, kwetu najisi,
(Najisi kwao, ni wema kwetu sisi:)
Ruka ukunguni, hewa tusitusi.

(*Wanaondoka.*)

### Onyesho 2. Kambi karibu na Forress

*Kamsa ndani. Wanaingia* **Dankan, Malkom, Donalben, Lenoksi,** *wakifuatana na wahudumu. Wanakutana na Sajini anayetoka damu.*

DANKAN: Mtu gani huyu atokaye damu? Anaweza,
Ionekanavyo hali yake, kutupa habari
Kamili ya hivi karibuni ya uasi huo.
MALKOM: Huyu ni yule sajini,
Ambaye, kama askari mwema na mshupavu,
Alinipigania kwa uhodari nisitekwe.
Karibu, rafiki shujaa! Mweleze mfalme
Hali ya mapigano hayo ulipotoka huko.
SAJINI: Yalikuwa katika hali ya mashaka mashaka;
Kama waogeleaji wawili waliochoka,
Wanaoshikamana na kufifisha ufundi wao.
Na Makdonald jahili—astahiliye
Kuwa mtu mwasi—na ili aweze kuwa hivyo,

Kapambika kwa maovu ya jadi y'ongezekayo—
Kapata msaada kwa visiwa vya magharibi,
Askari wenye silaha nyepesi na nzito.
Na Bahati, ikitabasamu na kusaidia
Uasi wake mlaanifu, ikajitokeza
Kama kahaba asiyetumainika wa mwasi:
Walakini hayo yote hayakumsaidia:
Makbeth shujaa—astahili sifa hiyo—
Akiibeza Bahati, na kupunga sime yake,
Ilotoa mvuke wa damu ya waliochinjwa,
Kama kipenzi cha uhodari kajipenyeza,
Kisha kamkabili huyo mtumwa wa Bahati:
Hakumpa mkono wa salamu, wala kwa heri,
Mara kamrarua kitovuni hadi shavuni,
Kichwa kakitundika kwenye pengo la buruji yetu.

DANKAN: O binamu yangu hodari! Mwungwana mashuhuri!

SAJINI: Kama mashariki, ambayo ni chanzo cha mwanga,
Huanza radi na dhoruba zivunjazo meli,
Kadhalika, palipotusadikishia faraja,
Pakabadilika kuwa chanzo cha kero jipya.
Sikiliza, mfalme wa Skotia, sikia:
Mara baada ya kujidhihirisha haki yako
Iliyofaidika kwa ujasiri wa Makbeth,
Na kuvikimbiza vikosi vya silaha nyepesi,
Mfalme wa Norwei, kuona 'wezekano,
Akiwa na silaha mpya na askari wapya,
Kaanza shambulio jipya.

DANKAN: Je, majemadari wetu, Makbeth na Banko,
Hawakuogofywa na shambulio hilo?

SAJINI (*akitabasamu kwa mzaha*): Ndiyo;
Ila kama zawaridi anavyomwogofya tai,
Au sungura, simba. Lakini nikisema kweli,
Nasema kwamba walionekana kama mizinga
Iliyoshindiliwa mitutu miwili; na hivyo
Wakashambulia adui huyo kwa nguvu kubwa:
Kama walitaka kuoga katika majeraha
Yaliyotoa mvuke wa damu ya mahasimu,
Au kukariri tukio lile la Golgotha,
Mimi siwezi kujua. Naona kizunguzungu,
majeraha yangu yamlalamikia tabibu.

DANKAN: Maneno yako yanaonyesha uhodari wako
Kama majeraha yako; na yote yadhihirisha
Heshima yako. Nenda, kamtafutie tabibu.

(*Sajini anaondoka, akisaidiwa na wahudumu.*)

Nani anakuja hapo?

*Anaingia Ross.*

MALKOM: Mtukufu na mheshimiwa Ross.
LENOKSI: Macho yake yanadhihirisha harara ya moyo!
Na hakika, inambidi kuonekana hivyo
Anayeleta habari ya kustaajabisha.
ROSS: Mungu amhifadhi mfalme!
DANKAN: Umetoka wapi, Sheki mtukufu?
ROSS: Natoka Fife, mfalme mkuu;
Ambako bendera za Kinorwei zapepea,
Zikitutaka shari na kuogofya watu wetu.
Na mfalme huyo wa Norwei binafsi,
Akiwa na lukuki ya askari watishao,
Ambao kapewa na yule haini, Sheki Kodo,
Alianza shambulio la kutisha. Mwishowe
Makbeth—kama mume wa Bellona katokea—
Na alipojivika deraya, alimkabili
Kwa ushupavu usiopata kifani po pote.
Wakapambana sime kwa sime, mkono, mkono,
Hatimaye kautiisha moyo wake safihi:
Hivyo ndiyo kusema ushindi ulikuwa wetu.
DANKAN: Furaha kubwa!
ROSS: Kwa sababu hiyo
Sasa Sweno, mfalme wa Norwei, ataka
Tumridhie mkataba wa kuleta amani;
Hatungemruhusu kuzika askari wake
Kabla ya kutulipa reale elfu kumi
Katika kisiwa cha Mtakatifu Kolmena,
Kwa matumizi ya jeshi letu zima.
DANKAN: Kamwe huyo Sheki Kodo hatatudanganya tena;
Nyoyo zetu haziwezi kuwa na imani naye:
Nenda kamtangazie hukumu ya kifo chake,
Kisha, kwa cheo chake, umsalimu Makbeth.

ROSS: Nitatimiza hivyo.
DANKAN: Alichopoteza, Makbeth mkuu kapata.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 3. Nyikani, karibu na Forres

*Ngurumo. Wanaingia wale* **wachawi** *watatu*

MCHAWI 1: Dadangu, umekuwapi saa zote?
MCHAWI 2: Nikiua nguruwe.
MCHAWI 3: Wewe je, dada, umekuwapi?
MCHAWI 1: 'Likutana na mke wa baharia,
Matunda pajani kayafurahia;
Akayatafuna, akayatafuna:—
"Nipe nami," ndivyo nilivyonong'ona:
"Toweka, mchawi," ndivyo kaniaga
Huyo mke mlafi mwenye vigaga.
Kaenda zake Aleppo mume wake,
Yu kapiteni wa Chui, meli yake:
Kwenye chekecheke nitaogelea,
Na, kama panya asiye na mkia,
Niitafune hata iharibike.
MCHAWI 2: Nitakupa upepo.
MCHAWI 1: Una huruma.
MCHAWI 3: Nami nitakupa Upepo mwingine.
MCHAWI 1: Nazimiliki hizo nyingine zote,
Na zinakovuma bandarini kote,
Pande zake zote, pia na majira,
Kama ionekanavyo kwenye dira.
Nitamkamua ukoka mkavu:
Usiku na mchana macho makavu,
Na kope zake za hanamu si hoja,
Hatalala usingizi lepe moja.
Budi aishi maisha ya upweke:
Majuma tisa fi tisa asumbuke,
Adhofu, akonde, na kunyong'onyea.
Ingawa meliye haitapotea,
Itajisukasuka kwenye tufani.

(*akiwaonyesha*)

Oneni nilicho nacho mkononi.

MCHAWI 2: Nionyeshe, nionyeshe.
MCHAWI 1: Ni dole gumba la nahodha wa meli,
Ambaye alivunjikiwa na meli
Akirejea makwao.

(*Ngoma yasikilika ndani.*)

MCHAWI 3: Huo mdundo wa ngoma!
Makbeth aja hima.
WOTE: Dada wa Ajali, ungeni mikono,
Kisha tuzungukezunguke, mfano
Wa wasafiri waendao kwa kasi,
Baharini na nchi kavu upesi:
Mizunguko mitatu yako, na tena,
Mingine mitatu yangu, na tena,
Mingine mitatu, itimie tisa.
Kimya! Uchawi 'mekamilika sasa.

*Wanaingia* **Makbeth** *na* **Banko.**

MAKBETH: Siku mbaya na njema kama leo sijaiona.
BANKO: Umbali gani umesalia kufika Forres?

(*akiwaona wale wachawi*)

Viumbe vilivyonywea, na mavazi kipekee,
Visivyofanana na viumbe vya ulimwenguni—
Na bado vyaonekana humo? Je mna uhai?
Au mwaweza mkawa kitu cho chote ambacho
Mwanadamu aweza kuhoji na kupata jibu?
Yaelekea ya kwamba mwatambua nisemayo,
Kwani nyote kwa pamoja mwaweka vidole vyenu
Viloatuka kwenye midomo iliyopooza:
Kwa maoni yangu, sura zenu shabaha ya kike,
Ila ndevu zenu zaniasa kusadiki hivyo.
MAKBETH: Neneni, kama mwaweza, ninyi ni viumbe gani?
MCHAWI 1: Salamu, Makbeth! O salamu, ewe Sheki wa Glamis!
MCHAWI 2: Salamu, Makbeth! O salamu, ewe Sheki wa Kodo!
MCHAWI 3: Salamu, Makbeth, utakayekuwa mfalme baadaye!
BANKO: Rafiki mtukufu, mbona unashtuka hivyo;

Waogopaje utabiri upendezao hivyo?
Katika jina la ukweli, niambieni kama
Ninyi ni sanamu tu au ni viumbe halisi—
Na kama maumbile yenu yanavyosadikisha?
Hapa mwenzangu mwamsalimu kwa cheo kipya,
Juu yake mkatabiri jambo kubwa zaidi,
Ndilo tumaini la kujipatia ufalme;
Na kwa hiyo anazielekea shabaha hizo.
Ila hamjataja lo lote kunihusu mimi:
Kama ninyi mwaweza kuagua mambo yajayo,
Na kujua mbegu iotayo na isiyoota,
Basi nambieni, mimi nisowaomba fadhili,
Wala kuogopa machukio yenu.

MCHAWI 1: Salamu!
MCHAWI 2: Salamu!
MCHAWI 3: Salamu!
MCHAWI 1: Kwa cheo, Makbeth atakuzidi,
Japo cheo chako kikubwa zaidi.
MCHAWI 2: Hutakuwa na furaha kama yeye,
Japo utafurahi kuliko yeye.
MCHAWI 3: Utakuwa mzazi wa wafalme,
Ila wewe hutakuwa mfalme.
Hivyo tunawapa heko,
Makbeth na Banko!
MCHAWI 1: Banko na Makbeth, pongezini!
MAKBETH: Ngojeni kwanza, enyi wenye usemi mbaya,—
Nielezeni zaidi: kwa kifo cha Sinelia,
Najua ya kuwa mimi ni Sheki wa Glamis:
Walakini vipi mnaniita Sheki wa Kodo?
Sheki Kodo mzima, mwungwana mwenye ufanisi;
Na uwezekano wangu kuupata ufalme,
Haufikiriki kamwe—wala haufikiriki
Zaidi ya 'wezekano wa kuwa Sheki wa Kodo.
Nambieni, mambo haya mwayapata toka wapi?
Au kwa nini mmechagua kutusimamisha,
Tukiwa katika nyika kame hii ya ukiwa,
Kutusalimu kwa utabiri wa jinsi hiyo?
Nijibuni, ninawaamuru!

(*Wachawi wanatoweka hewani.*)

BANKO: Yaelekea ardhi ina povu kama maji,
Na bila shaka, vitu hivyo ni povu la ardhi:
Wajua vimetoweka kwa upande gani?
MAKBETH: Hewani; na hayo maumbile tuliyoyaona
Yakayeyuka kama pumzi katika upepo.
Ningependa wakae hapa zaidi!
BANKO: Tuliviona vitu hivyo kwa macho yetu kweli?
Au tumekula mzizi uletao wazimu,
Na kuzifanya akili za watu zikawa butu?
MAKBETH: Watoto wako watakuwa wafalme.
BANKO: Nawe utakuwa mfalme.
MAKBETH: Pia Sheki wa Kodo: haikutabiriwa hivyo?
BANKO: Kwa sauti hiyo na maneno hayo. Nani huyo?

*Wanaingia* **Ross** *na* **Angasi.**

ROSS: Mfalme kapokea kwa furaha, Makbeth,
Habari za ushindi wako; naye anaposoma
Ujasiri wako binafsi kupinga waasi,
Mshangao wake na sifa akutunukiayo,
Hupingana kichwani na kuzidisha bumbuazi:
Kupumbazwa na mambo hayo, akayatafakari
Mengine yote yaliyotokea siku ya leo,
Kisha akakuona katika safu zenye nguvu
Za majeshi ya Norwei; wala hukuogopa
Ulichotenda mwenyewe, mfano unaotisha
Wa kifo hasa. Kwa mfululizo kama mvua,
Mjumbe baada ya mjumbe alikuja huko,
Na kila mmoja wao alileta sifa zako
Katika kuitetea milki ya mfalme,
Na wote wakaziwakilisha sifa hizo kwake.
ANGASI: Sisi tumetumwa
Kukupa shukrani za mfalme mtukufu;
Wajibu na fani yetu ni kukupeleka kwake,
Wala siyo kukupa tunzo.
ROSS: Ila sasa, ahadi ya cheo kikubwa zaidi,
Kan'amuru, mwenyewe, kukuita Sheki wa Kodo;
Basi kwa cheo hicho, salamu, Sheki mtukufu!
Hakika hicho ni cheo chako.
BANKO: Vipi, ibilisi anaweza kusema ukweli?

MAKBETH: Sheki wa Kodo angali anaishi:
Hivyo mbona wanivika magwanda yaloazimwa?
ANGASI: Yeye huyo aliyekuwa Sheki bado aishi;
Ila yu hai chini ya hukumu kali ya kifo,
Naye astahili kupoteza uhai huo.
Kama alijiunga na majeshi ya Norwei,
Au kama kwa siri alimsaidia mwasi,
Au yote mawili kuhatarisha nchi yake,
Mimi sielewi; ila wazi katenda jinaya
Istahiliyo kifo, nayo kakiri mwenyewe,
Ikathibitika na kumletea ma'ngamizi.
MAKBETH (*kando*): Sheki wa Glamis, na Sheki wa Kodo!
Bila shaka cheo kikubwa kuliko hivyo chaja.
(*akiwageukia Ross na Angasi*)
Ahosanteni kwa bidii yenu kunif'ata.
(*akimgeukia Banko*)
Hujaamini wanao watakuwa wafalme,
Ambapo walionIagia usheki wa Kodo
Hawakuwaahidi kingine ila ufalme?
BANKO: Ukiamini utabiri wao kikwelikweli,
Yumkini utatamani kupata ufalme,
Badala ya kutosheka na usheki wa Kodo.
Lakini hii ni ajabu kubwa: na mara nyingi,
Ili kutupa madhara, wajumbe hawa wa giza
Hututajia ukweli, na kutusadikisha
Ukweli huo kwa kutufunulia mambo duni,
Mradi watusaliti katika mambo makubwa.
(*akiwageukia Ross na Angasi*)
Binamu zangu, niwanong'onezeni, tafadhali.
(*Wanazungumza.*)
MAKBETH (*kando*): Ahadi mbili zimekwisha sadifu sawasawa,
Nazo ni matangulizi murua ya utukufu—
Upeo ambao kiini chake ni ufalme.—
Nawashukuru, waungwana.
(*kando*): Kichocheo hiki cha ajabu si kitu kibaya;
Wala hakiwezi kuwa chema: kama ni kibaya,
Mbona kimenipa matumaini ya ufanisi
Kwa kutabiri jambo ambalo limejiri sawa?
Hakika sasa nimekwisha kuwa Sheki wa Kodo:

Na kwa upande mwingine, kama kikiwa chema,
Niukubalije ushawishi huu wogofyao,
Unaozifanya nywele zangu zisimame wima,
Na hata kuufanya moyo wangu ulotulia
Unigongegonge mbavuni isivyo kawaida?
Hofu ya wakati huu haifikii kitisho
Cha mambo ninayoyafikiria ya baadaye:
Wazo langu, lililo uuaji fikarani tu,
Lanitisha na kuondoa harara ya kutenda,
Kwani fikara zangu zinaelemeza matendo,
Hata nayaona mambo yasiyopo kuwa yapo.

BANKO: Hebu oneni jinsi mwenzetu awazavyo.

MAKBETH (*kando*): Ikiwa bahati itanipa ufalme huo,
Basi, bahati itanitawaza bila juhudi.

BANKO: Bado hajavizoea hivyo vyeo vyake vipya,
Kama magwanda mapya yasivyotukaa mwilini
Mpaka tumeyavaa kwa muda mrefu.

MAKBETH (*kando*): Cho chote kitakachotokea fauwa,
Na ukipenda au usipopenda, litawika.

BANKO: Mtukufu Makbeth, tunakungojea wewe.

MAKBETH: Niwieni radhi, jamani: akili zangu butu
zilishughulishwa na mambo yalosahaulika.
Waungwana wema, kusumbuka kwenu kuja hapa,
Siku zote ni kumbukumbu katika moyo wangu.
Twendeni kwa mfalme.
(*akimgeukia Banko*)
Waza vema juu ya mambo haya yalotokea,
Na, tupatapo wasaa, tukisha yapima vema,
Tuzungumze pamoja kwa nyoyo zilizo safi.
(*Wanaondoka.*)

**Onyesho la 4. Forres. Jumba la Mfalme**

*Mdundo. Wanaingia* **Dankan, Malkom, Donalben, Lenoksi,** *na Wahudumu.*

DANKAN: Kodo amekwisha nyongwa?
Wajumbe nilowapa kazi hiyo hawajarudi?

MALKOM: Bwana wangu,
Hawajarudi bado. Lakini nimezungumza

Na mtu fulani alomwona kwa macho akifa,
Aliyeniambia Kodo kakiri kwa unyofu
Jinaya yake, na kaomba radhi ya mfalme,
Kisha akatubu kwa moyo: maisha yake yote
Hayakusifika kama jinsi ya kifo chake:
Alikufa kama mtu aliyezoea kufa,
Anayetoa kitu chake bora kuliko vyote,
Kama kwamba ni kitu duni kisicho na thamani.

DANKAN: Hamna njia maalum ya kuweza kujua
Fikara halisi za mtu kwa dalili za uso:
Yeye alikuwa mtu mwungwana na mwaminifu,
Na imani yangu kwake ilikuwa timilifu.

(*Wanaingia* **Makbeth, Banko, Ross,** *na* **Angasi.**)

O binamu mtukufu!
Dhambi yangu kutokukushukuru yanilemea;
Sifa yako hailingani na ujira wo wote.
Laiti hukuwa mstahiki jinsi hiyo,
Ningeweza kukujazi shukrani na ujira
Kadiri unavyostahili! Lakini kwa sasa,
Mambo yalivyo, siwezi kusema zaidi ila—
Vyote niwezavyo kukutuza, na hata zaidi,
Si linganifu na malipo unayostahili.

MAKBETH: Kutimiza wajibu na utii unipasao
Katika huduma yangu, ni ijara itoshayo;
Wajibu wa mfalme, kutudai utumishi:
Hakika, uhusiano kati ya wajibu wetu
Na mamlaka ya kifalme na nchi nzima,
Ni mfano wa ule ulio kati ya watoto
Na wazazi; na kati ya watumishi na mabwana;
Ambao budi wafanye yawapasayo kufanya,
Wakitimiza vyote kwa mujibu wa mapenzi
Na heshima yako.

DANKAN: (*akimkumbatia Makbeth na kumbusu*):
Nakukaribisha:
Nimeanza kukupandikiza, mfano mbegu,
Nikutunze ufikie upeo wa kukua.
Mtukufu Banko, usiyestahili machache
Kuliko huyu, na ambaye yapasa ijulike
Ya kuwa wewe u mstahiki kiasi hicho,

Nitakukumbatia, nikusogeze kifuani,
Uwe karibu zaidi na moyo wangu.

BANKO: Hapo nikikua, tunda litakuwa mali yako.

DANKAN: Furaha yangu isiyozuilika,
Yatafuta kujitokeza kwa njia ya machozi.
Wanangu, akraba zangu, waheshimiwa wangu,
Nanyi nyote mnaohusikana na kiti cha enzi:
Napenda mjue kwamba mtu atakayerithi
Mamlaka ya ufalme ni mwanangu mkubwa,
Malkom, ambaye tokea sasa tutamwita
Mwana Mfalme wa Kyumbalendi; na cheo hicho
Ni lazima kiambatane na vyeo vinginevyo,
Ili ishara ya utukufu, mithili ya nyota,
Ing'ae juu ya wastahiki wote.

(*akimgeukia Makbeth.*)

Twende pamoja kwenye ngome yako, Inverness,
Upate kutufadhili zaidi.

MAKBETH: Utumishi utachosha, usipokunufaisha:
Mimi nitawatangulia kama mpiga mbiu,
Na kuyafurahisha masikio ya mke wangu,
Kwa habari ya kufika kwako; naomba nondoke.

DANKAN: Vema, mtukufu wangu Kodo!

MAKBETH (*kando*): Mwana Mfalme wa Kyumbalendi! Au kikwazo
Hicho kitanifanya nijikwae na kuanguka,
Au nitaruka na kuuzidi upeo wake,
Kwani kimesimama njiani mwangu. Enyi nyota,
Ufichení mwanga wenu; huo mwanga usione
Nuksani yangu na hila iliyosetirika:
Jicho langu lisione mkono unachotenda;
Hata hivyo, na litendeke jambo hilo ambalo
Jicho huogopa kuliona linapotendeka.

(*Anaondoka.*)

DANKAN: Hakika, Banko mtukufu; yu shujaa mno,
Nami natosheka kabisa na sifa zake hizo;
Na sifa zake huniburudisha kama karamu.
Tumfuate aliyetangulia kuandaa:
Yeye ni ahali mwema, hamna kifani chake.

(*Mdundo. Wanaondoka.*)

## Onyesho la 5. Inverness. Ngome ya Makbeth

*Anaingia* **Bibi Makbeth** *akisoma barua.*

BIBI MAKBETH: Wachawi hao walionana nami siku ile ya ushindi; nami nina habari kamili ya kuwa wana uwezo unaozidi wa binadamu wa kufahamu mambo. Hawakukaa kuyajibu maswali yangu; kwani nilipokuwa na cheche za shauku ya kuwahoji zaidi, waliyeyuka na kutoweka hewani. Nikiwa nimesimama nikiajabia jinsi ya kutoweka kwao, wajumbe walinijia kutoka kwa mfalme, na kunisalimu rasmi, kama wale wachawi walivyofanya, kwa cheo cha 'Sheki wa Kodo.' Dada hao wa Ajali pia walinipongeza kwa 'Salamu utakayekuwa mfalme baadaye!' Nimeona yapasa sana kukupasha habari hizi, kwani wewe ni mwenzi wangu wa kwanza katika taadhima hiyo; na hivyo haistahili ukose hisa yako ya furaha, kutokana na kutokujua kwako utukufu ulioahidiwa. Yawazie mambo hayo vema; basi kwa sasa kwa heri.

(*Anafunga barua na kusema.*)

Tayari u sheki wa Glamis, na sheki wa Kodo;
Na budi utakuwa hicho ulichoahidiwa:
Lakini naogopa tabia yako; moyo wako
Una huruma kiasi ambacho hutathubutu
Kupitia njia iliyo fupi kuliko zote;
Ukuu waunolea meno, cheo watamani,
Lakini umepungukiwa na chembe ya uovu:
Upendacho kuliko vyote, wataka kukipata
Kwa njia adilifu; hutamani kufanya hila,
Walakini huwezi kufanikiwa bila hila:
Wapenda kukipata, ewe Glamis mkuu,
Kile kinachokushawishi, 'Yakupasa kutenda,
Kama wahitaji kukipata;' nalo tendo hilo
Uogopalo kutenda, hutalijutia kamwe:-
'Laiti halikutendeka', likiisha tendeka.
Harakisha kufika hapa, nikujaze ujuvi,
Kwa ujasiri wa ulimi wangu nivitiishe
Vyote vinavyokupinga usipate hilo taji,

Ambalo ajali na msaada wa miujiza
Vyaelekea kupendelea utawazwe kwalo.

(*Anaingia Mjumbe*)

Una habari gani?
MJUMBE: Mfalme atakuja hapa usiku wa leo.
BIBI MAKBETH: Una wazimu kusema hivyo!
Bwana wako hayupo naye?
Na kama kweli ndivyo,
Angalinionya nifanye matayarisho.
MJUMBE: Kunradhi, bibie, ni kweli: Sheki wetu aja:
Ila mjoli mwenzangu alimtangulia;
Ambaye, kuhema kifo, hakubakiwa pumzi
Inayotosha kuuwakilisha ujumbe wake.
BIBI MAKBETH: Mpe matunzo mema,
Aleta habari njema.

(*Mjumbe anaondoka.*)

Hata kunguru mwenyewe angepwewa na sauti,
Kama angalibashiri hatari ya Dankan
Ya kuingia chini ya buruji yangu. Njooni,
Enyi mizuka ya kuzimuni, mnaongojea
Mawazo ya kiuaji; niondoleeni uke,
Mnijaze farafara, unyayoni utosini,
Mawazo maovu ya kikatili kupindukia!
Gandisheni damu yangu, ziba njia ya majuto
Ili dhamiri yangu itokanayo na silika,
Isinifanye niogofywe na nia yangu hiyo,
Wala kujiingiza kati yake na utendaji!
Kikaribieni kifua changu chenye maziwa,
Na kisha badilini maziwa yangu yawe nyongo,
Enyi wajumbe wa mauaji mliojificha,
Po pote mlipo mkingojea tutende dhambi!
Njoo, usiku wenye giza zito, na jifunike
Kwa moshi mweusi kupindukia wa jehanamu,
Hata kisu changu kikali kisiweze kuona
Jeraha kifanyalo, na Mbingu isichungulie
Kwenye tabaka la giza na kuonya,
'Acha, Acha!'

(*Anaingia Makbeth*)

Glamis mkuu! Kodo mtukufu!
Mkuu hata zaidi, kwa cheo cha baadaye!
Barua zako 'menifunulia mambo yajayo,
'Meniondolea ujinga wa kutokufahamu,
Kwa hiyo fikarani, naishi wakati ujao.

MAKBETH: Kipenzi changu,
Dankan atakuja hapa usiku wa leo.

BIBI MAKBETH: Na ataondoka lini?

MAKBETH: Kesho, anavyotarajia.

BIBI MAKBETH: O kamwe
Jua halitaiona kesho hiyo!
Uso wako, Sheki wangu, ni mfano wa kitabu
Ambacho ndani yake waweza kusoma watu
Mambo ya ajabu. Ili kudanganya ulimwengu,
Budi uonekane kama watu wengine wote;
Jicho, mkono, ulimi, vionyeshe ukarimu:
Uonekane kama ua zuri, ila moyoni
Uwe kama joka lililojificha chini yake.
Huyo ajaye na apate anachostahili.
Nikabidhi kazi kubwa hiyo ya usiku huu,
Itakayokupa taji na mamlaka kamili,
Usiku na mchana, maisha yetu yote.

MAKBETH: Tutazungumza zaidi baadaye.

BIBI MAKBETH: Ila jibidishe uonekane mchangamfu;
Kubadili sura, daima ni ishara ya woga:
Viache vingine vyote mikononi mwangu.

(*Wanaondoka.*)

### Onyesho la 6. Mbele ya ngome ya Makbeth.

*Zomari na kurunzi. Wanaingia* **Dankan, Malkom, Donalben, Banko, Lenoksi, Makdaff, Ross, Angasi,** *na Wahudumu.*

DANKAN: Ngome hii imejengwa mahali pazuri mno;
Nayo hewa nyepesi inayotupuliza hapa
Inatuburudisha mwilini.

BANKO: (*Akimtazama mbayuwayu aliyejenga viota*)
Huyu mgeni wa kiangazi,
Aliyezoea kukaa katika mahekalu,
Athibitisha, kwa kujenga makao yake hapa,

Ya kuwa hewa hii hapa inavutia mno:
Katika kila kinundu, na juu ya kila picha,
Kiambazani, na kila nguzo ya ukuta wa nje,
Na katika kila pembe ifaayo kwa viota,
Pote ndege huyu kajitengenezea kitanda
Kining'iniacho na kiota kwa makinda yake:
Po pote ndege kama hawa wapendapo kukaa
Na kutaga mayai, jinsi nilivyochunguza,
Hewa ni nyepesi na nzuri.

(*Anaingia* **Bibi Makbeth.**)

DANKAN: Ona; mwone mkirimu wetu mtukufu!
Mapenzi tupewayo, aghalabu, huwa bughudha
Kwa wakirimu wetu; lakini inatulazimu
Kushukuru kwa mapenzi yaliyojitokeza.
Maana yake kusema hivyo ni kukufundisha,
Ututakie heri kwa kukutia mashughuli,
Na kutushukuru kwa masumbuko yako.

BIBI MAKBETH: Huduma yetu yote,
Hata ikifanywa mara mbili kwa kila njia,
Na kiisha ifanywe maradufu, hailingani
Na vyeo bora ulivyoiruzuku nyumba yetu:
Kutokana na vyeo vya zamani, navyo vya sasa,
Budi tuwe wahudumu chini ya fadhili zako.

DANKAN: Sheki wa Kodo yu wapi?
Tulikuja nyuma yake umbali mdogo sana,
Tukatarajia kufika hapa kabla yake:
Lakini yeye bingwa wa farasi; na mapenzi
Yake mengi kwetu, linganifu na wepesi wake,
Yalimwezesha kufika nyumbani kabla yetu.
Mkirimu adilifu, tu wageni wako leo.

BIBI MAKBETH: Daima tu watumishi wako; hivyo ni kusema
Sisi pamoja na watu wetu wote twafahamu
Watuaminisha wewe na maisha yetu haya,
Na riziki zetu; vyote vitumike upendavyo.
Tumelazimika kueleza kisa cha matendo
Na matumizi yetu saa yo yote upendayo,
Na kukurejeshea vile vilivyo mali yako.

DANKAN: Nipe mkono wako;
N'ongoze kwa mkirimu wangu: twampenda mno,

Na tutazidi kumtendea mambo ya hisani:
Kwa idhini yako, mkirimu mwema.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 7. Ngome ya Makbeth.

*Zomari na kurunzi. Anaingia Mpanga meza, na jamii ya watumishi wakiwa na masinia. Wanapita. Kisha* **Makbeth** *anaingia.*

MAKBETH: Kama mambo yangalikwisha tendo litendekapo,
Basi ingalikuwa murua litendeke hima:
Kama uuaji huu wa siri ungaliweza
Kunasa na kuelemeza tokeo lake ovu,
Na ukitimizika, unipletee ufanisi;
Laiti pigo hili moja lingekuwa tamati,
Na papo hapo lilete kikomo cha malipizi,
Hapa, penye ukingo hafifu wa maisha yetu,
Tusingejali adhabu ya baadaye peponi.
Walakini katika jinaya ya jinsi hii,
Sikuzote tuna adhabu yetu ulimwenguni;
Kwani twafundisha wengine siri ya mauaji,
Nao, waelewapo, humtendea vivyo hivyo
Yule alowafundisha. Hukumu hii ya haki,
Hutuwekea kikombe tulichokijaza sumu
Midomoni mwetu wenyewe. Kuwepo kwake hapa,
Ni kwa sababu ananiamini kwa njia mbili:
Kwanza, kwake mimi ni ahali na ni raia,
Na uhusiano huo walikanya tendo hilo;
Pili, kama mkirimu wake, nimelazimika
kupinga na kufungia wauaji wake nje,
Siyo mimi binafsi kumnyooshea sime.
Tena, Dankan ametawala kiadilifu,
Bila kushutumiwa katika mamlaka yake:
Naam, sifa zake hizo budi zimtetee,
Kama malaika wenye ndimi za matarumbeta,
Zikipinga jinaya hiyo ya kuuawa kwake:
Huruma, kama kitoto kichanga kilicho uchi,
Itaelea hewani, na malaika wa Mungu,
Anayebebwa na wajumbe wasioonekana,
Atatangaza tendo hilo ulimwenguni kote,

Mpaka machozi ya watu yazamishe upepo.
Sina kichocheo cha kunishawishi nilitende,
Isipokuwa tamaa yangu ya kupata cheo,
Ambayo ikizidi italeta maangamizi.

(*Anaingia* **Bibi Makbeth.**)

Vipi sasa! Waleta habari gani?

BIBI MAKBETH: Karibu amalize kula kilalio: kwa nini
Umetoka huko chumbani?

MAKBETH: Je, ameuliza niko wapi?

BIBI MAKBETH: Hufahamu kuwa kauliza?

MAKBETH: Hatutaendelea kutekeleza nia yetu;
Ni kitambo kidogo tangu anipe vyeo vipya,
Na kutokana navyo nimeheshimiwa na wengi;
Nitavifurahia vikiwa na thamani yake,
Na siyo kuvitupilia mbali mapema hivyo.

BIBI MAKBETH: Je, ni tumaini la kilevi
Lililokuchochea? Limekutia usingizini?
Na sasa lazinduka, likaduwaa na kupoa
Penye nia safii ya awali? Kutoka sasa
Mapenzi yako nayahesabu kigeugeu.
W'ogopa kuwa thabiti na shujaa wa matendo,
Kama ulivyo thabiti katika tamaa yako?
Wapenda kukipata kile unachokithamini
Kama kitu bora mno katika maisha yako,
Na kuishi kama mwoga penye tumaini lako,
Ukiruhusu woga kuitangulia tamaa,
Kama paka duni atajwaye katika methali?

MAKBETH: Tafadhali, kimya:
Nathubutu kutenda yampasayo mwanadamu;
Atakayethubutu kuzidisha, si mwanadamu.

BIBI MAKBETH: Basi ni hayawani gani
Aliyekufanya ukanieleza nia hiyo?
Wakati ulipothubutu kunuia jambo hilo,
Ndipo ulipodhihirisha uanadamu wako:
Na kama ungepata kilicho kikubwa zaidi,
Ungekuwa mwanadamu mstahiki zaidi.
Bila kuwa na wasaa na mahali pafaapo,
Wewe mwenyewe ulivitafuta vyote viwili:
Uwezekano kujitokeza, wewe waduwaa.

Mimi nimepata kunyonyesha, na ninafahamu
Mapenzi ya mama kwa kitoto kimnyonyacho:
Singekawia, hata kinichekeapo usoni,
Kuondoa titi langu kwenye fizi zake changa,
Nikiangushe na kuutapanya ubongo wake,
Kama niliweka nadhiri kumtendea hivyo,
Ulivyoweka wewe kulitimiza tendo hilo.

MAKBETH: Je, tukishindwa itakuwaje?

BIBI MAKBETH: Tukishindwa!
Kama ukipiga moyo konde, hatushindwi kamwe.
Dankan atakapolala usiku wa leo—
Na kwa uchovu wa safari atalala fofofo—
Nitawaandalia wahudumu wake wawili,
Karamu ya divai nyingi wapumbae kabisa,
Na kumbukumbu, inayohifadhi siri moyoni,
Ifumbwe, na ghala ya akili iwe kombe tupu:
Watakapolewa chakari na kulala kigogo,
Ni kitu gani ambacho wewe nami tutashindwa
Kumtendea huyo Dankan asiyelindwa
Au kuwabebesha walinzi wake walevi?
Hatia ya uuaji tutakaofanya sisi?

MAKBETH: Zaa watoto dume tu;
Kwani moyo wako mkakamavu hauruhusu
Ufunguke watoto wasiokuwa wanaume.
Haitakubalika, tukiisha wapaka damu
Hao wawili wa chumbani mwake waliolala,
Na baada ya kuzitumia sime hizo zao,
Kwamba ndio waliolitenda?

BIBI MAKBETH: Nani atakayethubutu kuamini vingine,
Hasa kwa kuwa tutapiga yowe la majonzi
Kwa ajili ya kifo chake?

MAKBETH: Nimeamua iwe hivyo, na nitanyoosha
Kila kiungo cha mwili wangu, kujitayarisha
Kwa tendo hilo la kutisha. Na twende zetu sasa,
Tukawadanganye watu kwa nyuso zetu kunjufu:
Uso wenye hila ufiche kile moyo ujuacho.

(*Wanaondoka.*)

# KITENDO CHA II

## Onyesho la 1. Kitalu cha ngome ya Makbeth.

*Wanaingia* **Banko** *na* **Flansi,** *akichukua kurunzi.*

BANKO: Sasa ni saa ngapi za usiku, mwanangu?
FLANSI: Mwezi umekwenda chini; na saa haijagonga.
BANKO: Na mwezi leo waenda chini saa sita.
FLANSI: Nadhani, Bwana, leo ni baada ya saa sita.
BANKO: Ngoja, chukua sime yangu. Mwanga unafifia,
Nyota za mbingu zimezimika zote. Lichukue
Na jambia hili pia. Nasikia usingizi,
Na bado nashindwa kulala: Mungu mwenye huruma,
Niepushe ndoto laanifu za usingizini!

(*Wanaingia* **Makbeth** *na Mtumishi mwenye kurunzi.*)

Nirudishie sime yangu.
Wewe hapo ni nani?
MAKBETH: Rafiki.
BANKO: Vipi, Bwana, hujapumzika bado?
Mfalme kaingia kitandani: kafurahi
Sana sana, na kwa ukarimu amewapa
Watumishi zawadi kubwa ya fedha: almasi
Hii kanambia nimsalimu nayo mkeo,
Kwa sifa anazostahili mkirimu mwema;
Naye kalala akiwa mwenye furaha kubwa.
MAKBETH: Minajili ya kupungukiwa na matayarisho,
Hatukuweza kumkirimu kama tupendavyo.
BANKO: Vyote vimetosha.
Usiku niliwaota wale wachawi watatu:
Kwako sehemu ya utabiri imejitokeza.
MAKBETH: Sipendi kuwafikiria:
Lakini, ikiwa tutaweza kupata wasaa,
Tutaweza kuzungumza mambo hayo zaidi,
Nayo yategemea kama utapata nafasi.
BANKO: Wakati wo wote upendapo.
MAKBETH: Ukiniunga mkono katika kusudi langu,
Hapo likitokea, nitakupa ustahiki.
BANKO: Ikiwa sipotezi heshima,
Nikijaribu kujiongezea ustahiki,

Na kama hatia itauambaa moyo wangu,
Nao uaminifu wangu haupati mkosi,
Nitakuunga mkono.

MAKBETH: Kwa sasa, nakutakia usingizi mwema!

BANKO: Ahsante sana, bwana: nawe lala unono!

(*Banko na Flansi wanaondoka.*)

MAKBETH: Kamwambie bibio, kinywaji kikiwa tayari,
Apige kengele. Kisha nenda zako ukalale.

(*Mtumishi anaondoka.*)

Je, hii ni sime ninayoiona mbele yangu,
Na mpini ukiukaribia mkono wangu?
Haya sogea, acha nikukamate mkononi.
Sijakupata, japokuwa bado ninakuona.
Huwezi kukamatika, ewe sime ya hatari,
Kama uwezavyo kuonekana wazi kwa macho?
Au u sime ya fikarani, mawazo ya hila,
Kutokana na akili zilizochochewa mno?
Bado nakuona, mwenye hali ya kukamatika,
Kama sime yangu hii nichomoayo alani.
Waniongoza njia niliyotarajia kwenda;
Na ambako ningetumia silaha kama hiyo.
Ama labda iwe macho yangu yadanganyika,
Na hivyo yazomewe na fahamu zangu nyingine,
La sivyo, yazidi milango mingine ya fahamu.
Bado ninakuona; na juu ya ubapa wako
Na mpini wako, matone ya damu yadondoka,
Na nilipokuona mwanzo, sikuona damu.
Yumkini sioni cho chote cha jinsi hiyo:
Fikara zangu za uuaji zadanganya macho.
Kwenye kizio chetu cha dunia, usiku sasa,
Na ndoto za uovu zamsumbua alalaye;
Wachawi wamhudumia Hekate kwa sadaka,
Na mwuaji wa kutisha, akifuata kamsa
Inayopigwa na mlinzi wake, mbwa-mwitu,
Aliye kama saa ya kumjulisha majira,
Analinyemelea windo lake kwa kimyakimya,
(Kama Tarquin alivyokinyemelea kitanda
Cha Lukretia kwa kusudi la kumbikiri.)
Ewe ardhi madhubuti ninayekukanyaga,

Usisikie mshindo wa miguu iendapo,
N'ogopa mawe ardhini yasije kunifeli,
Kisha kuurabishi wakati mtulivu huu
Ufaao mno kutekeleza kitisho hiki.
Nikitishia kwa maneno, atazidi kuishi:
Hakika, maneno matupu hayavunji mfupa,
Huipooza harara itafutayo matendo.

(*Kengele inalia.*)

Nakwenda; nalo litatendwa; kengele yaniita.
Usisikie, Dankan, kengele ipitayo
Ikwalikayo ama mbinguni ama jehanamu.

(*Anaondoka.*)

*Anaingia* **Bibi Makbeth.**

BIBI MAKBETH: Divai iliyowalevya imenipa ujuvi;
Kilichowaelemeza, kimenipa ushujaa.
Kimya! Sikiliza!
Huo ni mlio wa bundi utangazao kifo,
Na kutoa kwa heri ya mwisho ya kusikitisha.
Bila shaka, amekwenda kulitenda tendo lile:
Milango iko wazi; nao walinzi walevi
Wanaidhihaki kazi yao wanapokoroma:
Niliweka dawa ya kuwalevya kwenye divai,
Ili walale kigogo kama watu wafu.

MAKBETH (*ndani*): Nani huyo? Nini, ho!

BIBI MAKBETH: Maskini,
N'ogopa wameamka, na tendo halijatendwa:
Jaribio hili likishindwa tutaangamia.
Sikiliza! Nilitayarisha vema sime zao,
Na hangeweza kuzikosa. Na kama Dankan
Hakufanana na mzee wangu alipolala,
Ningemtendea tendo hilo.

*Anaingia* **Makbeth.**

Mume wangu!

MAKBETH: Nimetenda lile tendo. Hukusikia kelele?

BIBI MAKBETH: Nilisikia bundi na nyenje wakipiga mayowe.
Wewe hukusema?

MAKBETH: Lini?

BIBI MAKBETH: Sasa hivi.

MAKBETH: Nilipokuwa nikija chini?

BIBI MAKBETH: Ndiyo.
MAKBETH: Sikiliza!
Mtu gani kalala kwenye chumba kile cha pili?
BIBI MAKBETH: Donalben.
MAKBETH: Hii ni shani ya kusikitisha.
(*akiitazama mikono yake.*)
BIBI MAKBETH: Wazo la upuzi,
Kusema ni shani ya kusikitisha.
MAKBETH: Mmoja wao kacheka usingizini, mwingine
Kaomboleza, 'Uuaji!'
Na hivyo wakajiamsha: nikasimama pale
Na kuwasikiliza: Lakini waliomba dua,
Na halafu wakarudia kulala tena.
BIBI MAKBETH: Kuna wawili waliolala pamoja.
MAKBETH: Mmoja kasema 'Mungu tuhurumie!' 'Amina!'
*Mwenzake alijibu;*
Ikaonekana kama kwamba walitishwa mno
Na mikono yangu hii iliyotapakaa damu.
Nikiwa nikisikiliza mayowe yao ya woga,
Nikashindwa kutamka 'Amina!' waliposema
'Mungu tuhurumie!'
BIBI MAKBETH: Usijigonjweze kwa mawazo hayo.
MAKBETH: Lakini mbona nilishindwa kutamka 'Amina?'
Nilihitaji mno kupata huruma za Mungu;
Na 'Amina' ikanikwama kooni.
BIBI MAKBETH: Mambo haya hayahitaji kufikiriwa hivyo;
Au yatatufanya watu wehu.
MAKBETH: Nilidhani nilisikia sauti ikionya:
'Msilale tena!
Makbeth anaua usingizi,'—usingizi
Usio na hatia, unaoondoa uchovu,
Ulio kifo cha kila siku katika maisha,
Unaowaburudisha watu baada ya kazi,
Dawa maalum ya bongo zilizosononeka,
Kiburudisho cha pili, na sehemu mahsusi
Katika karamu ya maisha——
BIBI MAKBETH: Una maana gani?
MAKBETH: Sauti ikazidi kuonya 'Msilale tena!'
Na mwangwi wake ukaienea nyumba nzima:

'Sheki wa Glamis ameuua usingizi,
Kwa hiyo Sheki wa Kodo hawezi kulala tena;
Kamwe Makbeth hatalala tena.'

BIBI MAKBETH: Ni nani alilalamika jinsi hiyo? Mbona,
Sheki mtukufu,
Waficha uthabiti wako na kufikiria
Mambo kama ya kichaa? Nenda katafute maji,
Na unawe kuondoa ushahidi mkononi.
Mbona waziondoa sime hizi mahali pale?
Sharti ziwe pale: zichukue uzirudishe,
Na uwapake damu walinzi waliolala.

MAKBETH: Kamwe sitarudi pale:
N'ogopa hata kuliwaza tendo nililotenda;
Na sembuse kulitazama mara ya pili.

BIBI MAKBETH: Huna nia madhubuti!
Nipe sime hizo: walalao na waliokufa,
Ni mfano wa sanamu tu: ni jicho la mtoto
Liwezalo kutishwa na sanamu ya ibilisi.
Kama nikimkuta angali anatoka damu,
Nitazifanya nyekundu nyuso za walinziwe,
Kwa sababu budi hatia ionekane yao.
(*Anaondoka. Hodi kwa ndani.*)

MAKBETH: Sauti hiyo yatoka wapi?
Vipi leo, mbona kila sauti yaniogofya?
Mikono gani hii? Rangi yake yatisha macho!
Bahari ya Neptune yaweza kutakatisha
Mkono wangu ulioenea damu? Hapana,
Ni rahisi zaidi mkono huu kuifanya
Bahari kubwa yenye rangi ya kijani kibichi
Kuwa tabaka jekundu kubwa.

*Anaingia tena* **Bibi Makbeth.**

BIBI MAKBETH: Mikono yangu ina rangi nyekundu kama yako;
Lakini kuiogopa kama wewe ni fedheha.
(*Hodi kwa ndani.*)
Kuna mtu agongaye kwenye lango la kusini:
Twende chumbani. Maji kidogo yatatutakasa:
Jambo rahisi kiasi gani! Huna uthabiti.
(*Hodi kwa ndani.*)

Sikiliza! Kuna mtu anayezidi kugonga.
Vaa joho la kulala, tusije kutoka nje
Na kuonekana kama walinzi was'olala.
Mawazo yako yasikuletee huzuni hivyo.

MAKBETH: Kama kujikumbuka mwenyewe budi nikumbuke
Tendo nililotenda, basi heri nijisahau.

(*Hodi kwa ndani.*)

Haya mfufue Dankan kwa kugonga kwako!
Na laiti ungekuwa na uwezo kama huo!

(*Wanaondoka.*)

*Mahali papo hapo. Anaingia Bawabu, mlevi chakari.*

BAWABU: Lango lagongwa, naam! Kama mtu angekuwa bawabu wa Lango la jehanamu, angechoka mno kulifungua lango hilo.

(*Hodi kwa ndani.*)

Gonga, gonga, gonga! U nani wewe, katika jina la *Belzebub*? Bila shaka u mkulima aliyejinyonga kwa kuogopa kuwa mazao yangekuwa mengi kupita kiasi: hakika, umekuja wakati ufaao; njoo na leso za kutosha, kwani sharti utokwe na jasho hapa.

(*Hodi kwa ndani.*)

Gonga, gonga! Mtu gani wewe, kwa jina la yule ibilisi mwingine? Ah, budi awe mzandiki, aliyezoea kula yamini itatizayo: huapa ndiyo, na hapana, akijibu swali moja. Alifanya maasi ili ampendeze Mungu, lakini kushariti maneno kwake, hakukumfikisha mbinguni: O, ingia ndani, mzandiki.

(*Hodi kwa ndani.*)

Gonga, gonga, gonga! Na wewe ni nani? Aha, hapa kuna mshoni Mwingereza, anayestahili kuingia jehanamu, kwa ajili ya kuiba sehemu ya kitambaa alichopewa kushona suruali mtindo wa Kifaransa: ingia ndani, mshonaji; hapa pana joto la kutosha pasi yako ya kulainishia nguo.

(*Hodi kwa ndani.*)

Gonga, gonga! Hapa hakuna utulivu; na wewe ni mtu gani tena?

(*Bawabu anazinduka na kupata fahamu.*)

Lakini mahali hapa hapana joto kama jehanamu. Basi sitajidai kuwa bawabu wa ahera ya moto tena. Nilitarajia kuwafungulia lango la ahera watu wenye kazi mbalimbali, na wanaoishi raha mustarehe—wachomwe kwa moto uwakao milele na milele.

(*Hodi kwa ndani*).

Basi naja, naja sasa hivi! Tafadhali, nikumbukeni kwa bakshishi ya bawabu.

(*Anafungua lango.*)

*Wanaingia* **Makdaff** *na* **Lenoksi.**

MAKDAFF: Ulikesha sana, rafiki, hata ukachelewa
Kuamka kiasi hicho?
BAWABU: Kweli, bwana, tuliuchapa mtindi hadi jogoo la pili.
MAKDAFF: Bwana wako kaamka?

*Anaingia tena* **Makbeth.**

Kugonga kwetu kumemwamsha; huyo anakuja.
LENOKSI: Waamkaje, bwana mtukufu?
MAKBETH: Vema. Salamuni nyote.
MAKDAFF: Je, mfalme ameamka, Sheki mtukufu?
MAKBETH: Bado.
MAKDAFF: Alin'amuru nimwamshe asubuhi mapema:
Nasikitika kwa kuchelewa hivyo.
MAKBETH: Nitakuongoza alikolala.
MAKDAFF: Ingawaje nafahamu wapenda kuniongoza,
Sipendi kukusumbua; wacha niende mwenyewe.
MAKBETH: Kazi tunayoitamani, huponya maumivu.
Huu ndio mlango wa chumba alicholala.
MAKDAFF: Nitafanya utukutu kumgongea mlango,
Kwa sababu hii ni kazi aliyonikabidhi.

(*Anaondoka.*)

LENOKSI: Je, mfalme ataondoka leo?
MAKBETH: Ndiyo; ndivyo alivyotarajia.
LENOKSI: Usiku wa jana ulikuwa na rabsha nyingi:
Huko tulikolala, dohani zetu zil'angushwa
Kwa msukosuko wa dhoruba; isemekanavyo,

Vilio namna nyingi vilisikika hewani;
Sauti za ajabu kama ombolezo la kifo,
Zikitabiri kwa maneno yanayotisha mno,
Ghasia na machafuko yatakayoambatana
Na wakati huu wenye majonzi: pia bundi
Alilia usiku kucha: wengine wasema
Ardhi 'litetemeka kama mtu mwenye homa.

MAKBETH: Ulikuwa usiku wa machafuko.

LENOKSI: Katika ujana wangu, sijui kifani chake.

*Anaingia tena* **Makdaff.**

MAKDAFF: O kitisho, kitisho, kitisho! Ulimi na moyo
Haviwezi kukufikiria wala kukutaja!

MAKBETH: LENOKSI: Kuna nini?

MAKDAFF: Uharibifu umepata upeo wa ushindi;
Uuaji wa kikafiri mno umetokea,
Na kulidhuru lile hekalu teule la Mungu,
Ulipounyakua uhai wake,—

MAKBETH: Wasema nini? Uhai?

LENOKSI: Huyo umsemaye ni mfalme mtukufu?

MAKDAFF: Ingia chumbani, na budi utaharibu macho
Kwa shani itishayo: msingoje niwaeleze,
Nendeni mwone, kisha mseme ninyi wenyewe.

(*Wanaondoka Makbeth na Lenoksi.*)

Amkeni, amkeni!
Pigeni kamsa! Ni uuaji na uhaini!
Banko, Donalben! Malkom! amkeni!
Jipapatusheni usingizi ulio mtamu,
Mfano wa kifo, upakanao na kifo hasa!
Amkeni mwone taswira ya Hukumu Kuu,
Ambayo itatolewa siku ya kubaathiwa!
Malkom! Banko! Tokeni, kama kaburini:
Na halafu tembeeni kama mizuka, muweze
Kufanana na kitisho hiki! Pigeni kamsa.

(*Kengele inalia.*)

*Anaingia* **Bibi Makbeth.**

BIBI MAKBETH: Kuna shauri gani,
Ambalo limelazimisha kamsa kirihifu,
Inayowagutusha hao waliolala ndani?

Sema; niambie!

MAKDAFF: O bibie mwungwana,
Haifai usikie niwezacho kueleza:
Kukikariri katika sikio la mwanamke,
Ni kama kumwua kwacho atakapokisikia.

*Anaingia* **Banko**

O Banko, Banko,
Bwana wetu mtukufu ameuawa!

BIBI MAKBETH: Kitisho, maskini!
Wasema nini, katika nyumba yetu?

BANKO: Po pote, ni ukatili mkubwa.
Daff, mpendwa, nakuomba ujipinge mwenyewe,
Na kusema sivyo ilivyo.

*Wanaingia tena* **Makbeth** *na* **Lenoksi.**

MAKBETH: 'Ngekufa saa moja kabla ya tukio hili,
Ningeyahesabu maisha yangu furaha tupu;
Kwani toka sasa, hamna cha kustahilisha
Maisha ya binadamu: vyote ni mwanasesere:
Utukufu na ustahiki vimekwisha kufa;
Na mvinyo ya maisha imekamuliwa kau;
Masimbi yakaachwa, ulimwengu kujivunia.

*Wanaingia* **Malkom** *na* **Donalben**

DONALBEN: Kuna shauri gani?

MAKBETH: Umehasirishwa wewe, na bado hukufahamu?
Chemchemi ya damu yako imekwisha kaushwa;
Lile shina lake hasa ndilo lililokaushwa.

MAKDAFF: Mzee wako mtukufu ameuawa.

MALKOM: O, kauawa na nani?

LENOKSI: Ni hao wa chumbani mwake, ilivyoonekana;
Walitapakaa damu mikononi na nyusoni;
Pia na sime zao, ambazo hazikupanguswa,
Tulizikuta zimewekwa juu ya mito yao:
Wakatukazia macho kama wenye bumbuazi;
Haikupasa waaminishwe maisha ya mtu.

MAKBETH: O, hata hivyo, najutia mno ghadhabu yangu,
Ambayo ilinichochea hata nikawaua.

MAKDAFF: Kwa nini ulifanya hivyo?

MAKBETH: Kuna mtu gani awezaye kuwa na hekima,
Akili zinapomruka, au kuwa mpole,
Anapoghadhibika, au mwenye uaminifu,
Na bado aonekane maji ya uvuguvugu?
Hayupo: mapenzi yangu mengi kwa mfalme
Yalinipumbaza mno, nikarukwa na akili;
Kwa hiyo, sikusita na kupima nilichotenda.
Na kwa upande mmoja nilimwona Dankan,
Mwili wake mweupe ukiwa umepakwa damu,
Na kuonekana kama kipande cha nguo chenye
Rangi ya fedha, kilicho na ukanda wa dhahabu;
Nayo majeraha yake yakaonekana kama
Milango ya asili iliyokiingiza kifo.
Upande mwingine, nikaona wale wauaji
Wakitapakaa damu pote, na kuonekana
Kama watu ambao amali yao ni kuua!
Na sime zao zikavikwa mavilio ya damu,
Na kuonekana kama miguu iliyovikwa
Suruali inayochukiza. Hebu nambieni,
Mtu gani angeweza kujizuia, ikiwa
Ana moyo wa mapenzi, na kwenye moyo huo
Ushujaa wa kudhihirisha mapenzi yake?

BIBI MAKBETH: Nisaidieni nitoke nje, ho!

MAKDAFF: Mwangalie bibi huyo.

MALKOM (*kando kwa Donalben*): Mbona tunafyata ndimi zetu,
Na kumbe msiba huu ni wetu wenyewe?

DONALBEN (*kando kwa Malkom*): Twaweza kusema nini hapa,
Ambapo ajali yetu imekaa mafichoni,
Na yumkini itatimka kutushambulia?
Twende zetu; machozi yetu hayajajaa bado.

MALKOM (*kando kwa Donalben*): Wala jitimai yetu kubwa
Haijaufikia upeo wa kujitokeza.

BANKO: Mwangalie huyo bibi:

(*Bibi Makbeth anatolewa nje.*)

Na baada ya kuivika miili yetu nguo,
Ambayo sasa yapigwa na baridi, tukutane,
Na tulichunguze tendo hili ovu la maovu,
Mpaka tugundue chanzo na asili yake.
Hivi sasa twafadhaika kwa woga na mashaka:
Najiweka katika mikono ya Mungu mwenyezi,

Na ni tayari kuzipinga hila za mahaini.
MAKDAFF: Na mimi pia niko tayari.
WOTE: Nasi sote.
MAKBETH: Tufanye haraka kuvaa magwanda ya kivita,
Na sote pamoja tukutane katika kilinge.
WOTE: Umenena vema.

(*Wote wanaondoka ila Malkom na Donalben.*)

MALKOM: Utafanya nini? Kamwe tusitangamane nao:
Kuonyesha huzuni ya uongo ni jambo rahisi
Kwa mtu wa hila. Nitakimbilia Wingereza.
DONALBEN: Nami Ayalendi; tukienda pande tofauti,
Tutaongeza uwezekano wa kusalimika:
Hapa vicheko vya watu vinazisetiri sime:
Na kikulacho ki nguoni mwako.
MALKOM: Mshale huo uliofyatuliwa,
Haujaifikia hatima ya shabaha yake,
Na usalama wetu ni kukwepa shabaha hiyo.
Hivyo tupande farasi zetu; tusilimatie,
Wala kujicheleweshe hapa kwa matayarisho,
Ila tutitimke mapema iwezekanavyo:
Hakika, tunatoroka kama wezi, walakini
Inakubalika hata wezi kutoroka hivyo—
Ikiwa hamna hata chembe moja ya huruma.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 2. Nje ya Ngome ya Makbeth.

*Wanaingia* **Ross** *na* **Shaibu.**

SHAIBU: Miaka yangu sabini nakumbuka barabara:
Na katika muhula mrefu huo nimeona
Nyakati zenye vitisho, na mambo ya kiajabu;
Ila rabsha ya usiku huu yazidi hivyo.
ROSS: Ah, baba mwema,
Unaiona mbingu ikifutuka kwa ghadhabu,
Kwa ajili ya matendo maovu ya binadamu,
Nayo yaonya jukwaa la damu la ulimwengu:
Kwa majira ya saa kumekucha, lakini giza
Lauelemeza mwanga wa taa itembeayo:
Je, tuseme ni kwamba usiku washinda mchana,

Au kwamba mwanga wa mchana unatahayari,
Ndiyo giza likaufunika uso wa dunia,
Ambapo nuru inayohuisha ingeubusu?

SHAIBU: Hiyo ni ajabu,
Kama na ajabu ya tendo hilo lililotendwa.
Jumanne iliyopita, kipanga aloruka
Angani upeo wa juu kama alivyoweza,
Kashambuliwa na kuuawa na bundi ambaye,
Kwa jadi yake, hula mapanya mwitu.

ROSS: Na farasi wa Dankan—jambo la ajabu na la hakika—
Wenye maumbile mema na wenye kwenda kasi,
Naam, kiolezo kikamilifu cha farasi,
Waligeuka farasi mwitu, wakavunja kuta
Za mazizi yao, na kisha wakapiga mateke,
Kisha kukataa kuwatii masaisi wao,
Kama kwamba kuwataka shari binadamu wote.

SHAIBU: Yasemekana walilana wenyewe kwa wenyewe.

ROSS: Walitenda hivyo, kuyaajabisha macho yangu
Yaliyowaangaza. Namwona Makdaff aja.

*Anaingia* **Makdaff**

Naam, bwana, mambo yakoje sasa?

MAKDAFF: Swali gani hilo; huwezi kuyaona mwenyewe?

ROSS: Je, amejulikana aliyefanya uuaji
Huu unaozidi mauaji ya kawaida?

MAKDAFF: Ni hao ambao Makbeth kawachinja.

ROSS: Masalale!
Walitegemea kujipatia faida gani?

MAKDAFF: Walichochewa:
Malkom na Donalben, wana mfalme,
Wametoroka na kukimbilia nchi za mbali,
Kitendo ambacho chaonyesha lawama ni lao.

ROSS: Ajabu nyingine!
Kupenda cheo kusikoleta faida yo yote,
Na kunakoangamiza shina la maisha yake!
Basi, bila shaka, ufalme ni wa Makbeth.

MAKDAFF: Ametajwa; na amekwenda Skone kutawazwa.

ROSS: Maiti ya Dankan iko wapi?

MAKDAFF: Imepelekwa Kolmekili,
Katika kaburi takatifu la mababu zake,

Linalohifadhi mifupa yao.
ROSS: Je, utakwenda Skone?
MAKDAFF: La, binamu yangu, nitakwenda Fife.
ROSS: Vema, mimi nitakwenda huko.
MAKDAFF: Vizuri, napenda upate kila la heri huko:
Kwa heri! Hatujui kama magwanda yetu mapya
Yatatuchukua vema kama yetu ya zamani!
ROSS: Kwa heri, mzee wangu.
SHAIBU: Mungu na awabariki ninyi, pamoja na wote
Wan'ojaribu kubadili uovu kuwa wema,
Na mahasimu kuwa marafiki!

(*Wanaondoka.*)

## KITENDO CHA III

### Onyesho la 1. Forres. Jumba la Mfalme

*Anaingia* **Banko**

BANKO: Una vyote sasa: ufalme, usheki wa Kodo,
Usheki wa Glamis, vyote walivyobashiri
Wale Dada wa Ajali. Lakini, nina mashaka,
Ulifanya hila kuifikia shabaha hiyo:
Lakini walitabiri, taji halitaselea
Katika nyumba yako, kurithiwa na wajukuu,
Kwa sababu mimi nitakuwa mzizi na baba
Wa wafalme wengi. Ikiwa huo ni ukweli—
Na kwako wewe, Makbeth, vyote ni dhihirifu—
Kwa nini, kama ukweli umejitokeza kwako,
Wasiyatabiri yaliyo ya kweli juu yangu,
Na kunitumainisha? Kimya! Sisemi zaidi.

*Unasikika Muziki unaomtangulia mfalme mpya. Kisha wanaingia* **Makbeth,** *kama mfalme,* **Bibi Makbeth,** *kama malkia,* **Lenoksi, Ross,** *Makabaila wa Skotia, Mabibi, na Wahudumu.*

MAKBETH: Huyu ndiye mgeni wetu wa heshima.
BIBI MAKBETH: Kama alisahaulika,
Basi karamu yetu kubwa leo haingefana,
Na tamasha yote haingeweza kukamilika.
MAKBETH: Usiku wa leo, bwana, tuna karamu rasmi,
Na kuwepo kwako ni furaha yangu.

BANKO: Wajibu wako, mfalme mkuu,
Ni kuniamuru; na wajibu unaonipasa,
Ni kukutii kwa uaminifu mkamilifu,
Daima dawamu.
MAKBETH: Alasiri hii utatoka kupanda farasi?
BANKO: Ndiyo, bwana wangu mwema.
MAKBETH: Tungalipenda kupata mashauri yako bora
Katika baraza ya leo; na mawaidha yako
Kila mara yamekuwa bora na yenye faida;
Lakini twaweza kuahirisha mpaka kesho.
Je, watarajia kwenda mbali kwa farasi wako?
BANKO: Nitakwenda mbali iwezekanako kufika,
Kati ya sasa na wakati wa kula kilalio:
Na kama farasi wangu hakufungulia mwendo
Kuliko ilivyo kawaida yake, itanibidi
Kurudi saa au mbili baada ya machweo.
MAKBETH: Usiikose karamu ya taifa, tafadhali.
BANKO: Habibi wangu, sitaikosa.
MAKBETH: Tumesikia kuwa binamu zangu wauaji
Wamekimbilia Uingereza na Ayalendi,
Ambako wasakini bila kutubu dhambi yao
Ya kumwua mzee wao; na huko waongopa
Mambo kadha wa kadha, na yote ya uzushi wao.
Lakini jambo hilo tutalizungumza kesho,
Tutakapoyajadili mambo ya taifa letu.
Basi nenda kwenye matembezi yako: buriani,
Mpaka tuonane tena urudipo usiku.
Je, Flansi atakwenda pamoja nawe?
BANKO: Naam, habibi wangu: na wakati umetimu.
MAKBETH: Natakia farasi wenu mbio na usalama;
Na hivyo pandeni farasi hao na kuondoka.
Buriani.

(*Banko anaondoka.*)

(*Akiugeukia msoa wake.*)

Kila mmoja aweza kufanya anachopenda
Mpaka itimiapo saa moja ya usiku;
Na hadi wakati huo napenda kuwa mwenyewe,
Ili nifurahi upya tukutanapo jioni:
Basi, mpaka wakati huo, Mungu awe nanyi!

(Wote wanaondoka, ila *Makbeth* na Mhudumu)
Kitwana wee! Napenda kuuliza neno moja:
Je, watu hao wanangojea niwape amri?
MHUDUMU: Ndiyo, habibi wangu; wanangojea nje ya lango.
MAKBETH: Walete mbele yangu.

(*Mhudumu anaondoka.*)

Cheo hiki pekee si kitu:
Ubora ni kuwa nacho pamoja na usalama.—
Hofu yetu kwa Banko ina msingi imara;
Staha yake ya kifalme inaogopesha:
Yu shujaa mno: na, zaidi ya moyo hodari,
Ana hekima ya kuongoza ushujaa wake,
Ili kila atendacho kitendeke kwa salama.
Maisha ya mtu mwingine s'ogopi, ila yake;
Na, mbele yake, hata malaika anilindaye,
Hutetemeka kwa woga: kama isemekanavyo,
Yule wa Marko Antoni alitetemeka
Mbele ya Kaisari. Aliwagombeza wale dada,
Siku ile ambayo walinitaja mfalme,
Akawaamuru kuagua ufanisi wake;
Wakatabiri atakuwa baba wa wafalme:
Kichwani mwangu wakaliweka taji lipitalo,
Na mkononi mwangu, fimbo nitakayonyang'anywa,
Makusudi itukuze wasio wa mbari yangu,
Nao wanangu wasije kuurithi ufalme.
Kama ndivyo ilivyo, nimenajisi moyo wangu
Kwa faida ya wana Banko; kwa ajili yao,
Nikamwangamiza yule Dankan mtukufu,
Na kukijaza sumu kikombe changu cha amani;
Na roho yangu idumuyo milele na milele,
Nikampa ibilisi, adui wa binadamu.
Loo! Kwa madhumuni ya kuwafanya wafalme!
Mbegu za Banko zisitawi kuwa wafalme!
Kuliko iwe hivyo, naitaka shari ajali,
Tukabiliane kivita, kifo kituamue!
Nani huyo?

(*Anaingia tena Mhudumu akifuatana na Wauaji wawili.*

Sasa nenda mlangoni, ungoje nikuite.

(*Mhudumu anaondoka.*)

Si ilikuwa jana tulipoongea pamoja?

MWUAJI 1: Ndiyo, mfalme mtukufu.

MAKBETH: Basi vema; sasa
Mmelifikiria jambo nililowaeleza?
Kumbukeni ya kuwa ndiye aliyewadhulumu,
Nanyi mkadhani ni mimi nisiye na hatia:
Jambo hilo niliwaelezeni kinaganaga
Kwenye mazungumzo ya jana, nikawaonyesha
Jinsi mlivyopingwa na kuhadaiwa, hila
Aliyotumia, watu waliomsaidia,
Na mambo mengineyo yote ambayo yangeweza
Kumhakikishia mtu afkani na mwehu
Kuwa "Banko kafanya kadhaa."

MWUAJI 1: Ulitufunulia jambo hilo.

MAKBETH: Kweli ndivyo, na pia niliendelea zaidi;
Hii ndiyo sababu ya kukutana tena loe.
Je, una uvumilivu wa jadi kiasi gani,
Hata usafii huo upite bila kujali?
Je, unaamini mno msamaha wa Injili,
Hata umtakie baraka mtu mwovu huyo
Na watoto wake, ambaye amekuelemeza
Kwa mkono mzito, ukachungulia kaburi;
Nawe na jamaa kutegemea zaka milele?

MWUAJI 1: Sisi ni wanadamu, mfalme wangu.

MAKBETH: Naam, katika orodha ninyi ni wanadamu;
Kama na mbwa wa kawaida, na mbwa wembamba,
Mbwa sariama, na mbwa wa manyoya marefu
Na masikio marefu; kimbwa cha mbegu duni,
Na mbwa mkubwa wa manyoya ya matimtimu,
Mbwa wapigao mbizi, na mbwa-mwitu sariama,
Wote hujumlishwa katika orodha ya mbwa:
Jedwali inayozitambua sifa tofauti,
Hutenganisha mbwa wepesi na wale wazito,
Wakali, na wapole; wa nyumbani, na wa kuwinda:
Kila mmoja kwa mwujibu wa vipawa ambavyo
Ukarimu wa jadi umemjazi; na kwa hiyo,
Anatambulikana kwa jina lake maalum,
Badala ya wote kuwekwa kwenye orodha moja:
Hali kadhalika, ndivyo ilivyo kwa binadamu.

Kama una cheo mahsusi kiambatanacho
Na sifa zako fulani fulani, na ukitaje,
Na ikiwa cheo hicho si duni kuliko vyote,
Nitakukabidhi kazi hiyo uikamilishe.
Ikifanyika, itakuondolea adui yako,
Na ikuvute moyoni na mapenzini mwetu.
Yeye aishipo, siha yetu shuti iwe nyonge,
Ila angalikufa, tungekuwa wakamilifu.

MWUAJI 2: Mimi ni mmoja, mfalme wangu,
Ambaye mapigo na masumbuko ya ulimwengu
Yamenikasirisha kiasi cha kutokujali
Ninachotenda kuutolea chukiulimwengu.

MWUAJI 1: Nami ni mwingine
Niliyeteseka, nikavuta kamba na bahati,
Na sasa ninangojea uwezekano wo wote,
Niyasitawishe maisha ama niyakomeshe.

MAKBETH: Nyote wawili
Mnajua Banko alikuwa adui yenu.

WAUAJI: Kweli, bwana wangu.

MAKBETH: Kwangu pia yu adui, na kuwa karibu naye
Ni hatari kubwa: nayaogopa maisha yake,
Hata ya dakika moja, kama kichomi cha sime
Ubavuni mwangu: na ingawaje nina uwezo,
Kumwondoshea mbali kwa kutumia mamlaka,
Na kusema afe kwa amri yangu, sithubutu,
Kwani kuna marafiki fulani wangu na wake,
Ambao sipendi kuwaudhi; hivyo ingebidi
Niomboleze juu ya niliyemwua mwenyewe:
Ni kwa sababu hiyo nawaombeni msaada,
Jicho la hadhara lisione hila yangu hiyo,
Kwa sababu fulani maalum nilizo nazo.

MWUAJI 2: Tu tayari, bwana wangu,
Kufanya jambo lo lote utakalotuamuru.

MWUAJI 1: Hata kama maisha yetu—

MAKBETH: Sasa mwaonyesha uhodari. Baada ya muda
Usiozidi saa moja, nitawafahamisha
Mahali pazuri pa kujificha na kuotea;
Kisha doria awape ishara ili mjue
Wakati na saa hasa ya kutenda tendo hilo;
Kwani sharti litendeke usiku huu huu,

Nalo litendeke mbali na jumba la mfalme;
Watu wasije wakanitilia shaka yo yote.
Pamoja naye—ili kazi yenu ikamilike—
Mwanaye Flansi, anayefuatana naye,
Na maisha yake yan'tisha kama ya babiye,
Yambidi aibusu ajali ya giza hilo.
Sasa tokeni na kushauriana jambo hilo:
Nitawaiteni baadaye.

WAUAJI: Tumekwisha kata shauri, bwana wangu.

MAKBETH: Nitawaiteni sasa hivi: kaeni karibu.

(*Wauaji wanaondoka.*)

Imeamuliwa: Banko, ikiwa roho yako
Yaenda mbinguni, itafika usiku wa leo.

(*Anaondoka.*)

**Onyesho la 2. Jumba la Mfalme.**

*Wanaingia* **Bibi Makbeth** *na Mtumishi.*

BIBI MAKBETH: Banko ametoka kwenye jumba la mfalme?

MTUMISHI: Ndiyo, bibie, lakini atarudi usiku.

BIBI MAKBETH: Mwambie mfalme ningependa kusema naye.

MTUMISHI: Bibie, nitamwambia.

(*Mtumishi anaondoka.*)

BIBI MAKBETH: Hamna faida:
Ni hasara kupata matakwa bila kutosheka:
Ni heri tungekuwa huyo tuliyemwangamiza
Kama kwa kifo chake tutapungukiwa furaha.

*Anaingia* **Makbeth.**

Vipi, bwanangu! Mbona wapenda kukaa kitwea,
Na kufanya mawazo yatishayo mwenzi wako;
Ukayahifadhi mawazo ambayo ilibidi
Yafe na mtu huyo yanayohusikana naye?
Mambo yasiyo na maponyo si vema kuyajali:
Kilichotendeka kimetendeka.

MAKBETH: Tumelijeruhi joka, bali hatukuliua:
Jeraha litapona, arudiwe na hali yake;
Nasi, na usafihi wetu ulio kazi bure,
Tuwe kwenye hatari ya jino lake la zamani:
Lakini hata kama ulimwengu ukichanika,

Naam, hata mbingu na nchi zikiangamia,
Haitatubidi kula katika hali ya woga,
Wala kulala tukisumbuliwa na jinamizi
Linalotufanya tutetemeke kila usiku:
Laiti tungekuwa na marehemu kaburini,
Ambaye sisi, ili kujiongezea furaha,
Tumempa pumziko na amani ya daima,
Kuliko kukesha na mateso makali moyoni.
Sasa Dankan yuko kaburini; na baada
Ya kiherehere cha maisha, amelala kimya;
Uhalifu umetenda jambo kubwa uwezavyo:
Wala sime, wala sumu, na wala mahasimu wa
Humu nchini, wala majeshi yatokayo nje—
Cho chote—hamna kiwezacho kumdhuru tena.

BIBI MAKBETH: Basi, yatosha;
Bwanangu mwema, onyesha uso unaonawiri;
Na pia uwe mwenye furaha na kutabasamu,
Mbele ya wageni mashuhuri usiku wa leo.

MAKBETH: Vema, mpenzi; nawe pia jitahidi hivyo:
Tena umvike Banko kilemba cha ukoka;
Uso na maneno vimsadikishie heshima:
Yabidi tujidhili, tutumie urairai,
Nao ucheshi wa nyuso zetu uwe kifuniko
Cha mioyo yetu kuficha hali yake halisi,
Kwani makao yetu hayajakamilika bado.

BIBI MAKBETH: Yakupasa kusahau mambo hayo.

MAKBETH: O mke wangu halili, mawazo yangu yachoma
Mithili ya kichomi cha nge. Watambua ya kuwa
Banko na Flansi mwanawe bado wa hai!

BIBI MAKBETH: Kweli; walakini hawawezi kuishi milele.

MAKBETH: Bado kuna matumaini; waweza kudhurika;
Katika tumaini hilo waweza kufurahi:
Usiku wa leo, kabla popo hajadiriki
Kuzunguka matao; naam, kabla ya mende
Wadogo kutoa mvumo kwa mbawa zao changa,
Wakiitikia wito wa Hekate, malkia
Wa usiku atishaye, 'kitukumbusha kulala,
Tendo kubwa linalotisha litakwisha tendeka.

BIBI MAKBETH: Ni jambo gani hilo litakalotendeka?

MAKBETH: Mpenzi wangu, usipende kulijua sasa,

Na mpaka litendeke ndipo ulishangilie.
Njoo, ewe usiku wenye giza lililo zito,
Ulifunike jicho la mchana lenye huruma;
Kwa mkono wako katili usioonekana,
Ondoshea mbali hicho kinachonipa unyonge!
Giza laingia, kunguru waanza kurudi
Mwituni kwenye viota vyao: viumbe wazuri
Wa mchana wa'nza kuchoka na kusinzia,
Na udhalimu wa giza wawinda mawindo yake.
Waajabia maneno yangu: lakini tulia;
Msingi dhalimu, husitawishwa kwa udhalimu.
Kwa hiyo, tafadhali nifuate.

(*Wanaondoka.*)

**Onyesho la 3. Bustanini karibu na jumba la mfalme.**

*Wanaingia Wauaji watatu*

MWUAJI 1: Lakini nani kakwambia uchangamane nasi?
MWUAJI 3: Makbeth.
MWUAJI 2: Haipasi tumtilie shaka; anakariri
Kazi ile ile tuliyohitaji kutenda,
Na kwa mwujibu wa maagizo tuliyopokea.
MWUAJI 1: Basi changamana nasi.
Miale ya jua bado yaonekana magharibi:
Sasa msafiri alochelewa aharakisha
Farasiwe ili asije kuguiwa na giza
Kabla ya kufikia hatima ya safariye;
Na huyo tunayemngojea sasa yu karibu.
MWUAJI 3: Sikiliza! Nasikia mwendo wa farasi.
BANKO (*ndani*): Ninyi hapo, tumulikieni, ho!
MWUAJI 2: Bila shaka ndiye: wengine wote waloalikwa
Wamekwisha fika kitambo na wameketi ndani.
MWUAJI 1: Farasi wake huzungukazunguka.
MWUAJI 3: Kuzunguka kote huko ni kama maili moja:
Ila, kwa kawaida, kama watu wengine wote,
Hupita njia hii fupi kulifikia lango.
MWUAJI 2: Mwenge, mwenge!
MWUAJI 3: Ndiye.

(*Wanaingia* **Banko,** *na* **Flansi** *akiwa na mwenge*).

MWUAJI 1: Simameni imara.

BANKO: Mvua zitanyesha usiku wa leo.
MWUAJI 1: (*akimrukia Banko*): Acha zikunyeshee.
(*Wote wanamshambulia.*)
BANKO: O uhaini! Hima kimbia, Flansi mwema,
Kimbia, kimbia, kimbia! Labda utaishi
Na kulipiza kisasi. O mshari!
(*Anakufa. Flansi anatoroka.*)
MWUAJI 3: Nani aliyezimisha mwenge?
MWUAJI 1: Haikupasa hivyo?
MWUAJI 3: Ni mmoja tu kaanguka; mwanawe katoroka.
MWUAJI 2: Kazi yetu 'mepoteza sehemu kubwa zaidi.
MWUAJI 1: Basi, twendeni, tuseme tulodiriki kutenda.
(*Wanaondoka.*)

**Onyesho la 4. Mahali papo hapo.**

*Chumba katika jumba la mfalme. Karamu imetayarishwa.*

*Wanaingia* **Makbeth, Bibi Makbeth, Ross, Lenoksi,** *Waheshimiwa na Wahudumu.*

MAKBETH: Kaeni kwa mujibu wa daraja za vyeo vyenu:
Nami ninawakaribisheni nyote kwa jumla.
WAHESHIMIWA: Ahsante, mfalme mtukufu.
MAKBETH: Mimi binafsi nitatangamana nanyi nyote;
Nitawakirimu kama mkaribishaji wenu.
Malkia yu kando, kakalia kiti cha enzi,
Ila baadaye, nitamwomba awakaribishe.
BIBI MAKBETH: Naomba, bwana, wakaribishe kwa niaba yangu,
Na mimi nawasalimu katika fuadi yangu.
(*Mwuaji* 1, *atokea mlangoni.*)
MAKBETH: Ona wanavyoyakubali makaribisho yako
Kwa mioyo ya shukrani. Watu walivyokaa,
Pande zote mbili za meza zina idadi sawa,
Nami nitaketi hapa katikati: furahini,
Na kujilisi mpendavyo; halafu tutakunywa,
Tumtakie kila mmoja hapa siha njema.
(*Anakwenda mlangoni.*)

Naona damu usoni pako.

MWUAJI: Basi sharti iwe ya Banko.

MAKBETH: Bora damu yake kuonekana usoni pako
Kuliko yeye kuwa hapa. Je, amekwisha kufa?

MWUAJI: Bwana, koo lake limekatwa; ndimi nilokata.

MAKBETH: Umewazidi wote wenye amali ya kuchinja:
Alomchinja Flansi, pia ni msifiwa;
Kama ndiwe, ushupavu wako hauna kifani.

MWUAJI: Bwana mwenye taadhima, Flansi katoroka.

MAKBETH: Basi kama ndivyo, hofu yangu imerudi tena:
Na kama sivyo, ningalikuwa salama kabisa,
Makao yangu yawe imara kama marmar,
Na msingi, kama mwamba unaoenea pote,
Mithili ya hewa inayotuzunguka. Walakini
Sasa najiona nimefungwa na kutawaliwa,
Nikafunikwa gubigubi kwa hofu na mashaka.
Lakini Banko kafa?

MWUAJI: Ndiyo, habibi mkuu: kalala kwenye handaki,
Na kaenezwa majeraha ishirini kichwani,
Na hata lile dogo ya yote laweza kuua.

MAKBETH: (*kando*): Ahsante kwa hayo:
Joka hilo limelala hapo; na kitoto chake
Kilichokimbia kina jadi ya kutoa sumu,
Walakini kwa sasa hakijaota meno bado.

(*Akimgeukia Mwuaji*).

Waweza kwenda sasa: kesho tuzungumze tena.

(*Mwuaji anaondoka.*)

BIBI MAKBETH: Bwanangu, huonyeshi ukarimu upasao:
Karamu kufana, yapasa makaribisho mema,
Bila hivyo, itaonekana imenunuliwa;
Kama karamu ni kula tu, basi, bora nyumbani;
Karamuni, ukarimu ndiyo ladha ya chakula,
Usipopatikana, budi karamu iwe dufu.

MAKBETH: Mpenzi, umenikumbusha!
Nawatakieni tamaa nzuri ya chakula,
Kiwapendeze mwilini, na kuwapa siha njema!

LENOKSI: Bwana mtukufu, kwa mapenziyo, keti sasa.

(*Mzuka wa Banko unaingia na kukalia kiti cha Makbeth.*)

MAKBETH: Nyumba yetu ingalijaliwa utukufu mwingi,
Kama Banko wetu adhimu alikuwa nasi,
Na ambaye naona ni rahisi kumshutumu,
Kwa kufanya kusudi na kukataa kuja hapa,
Kuliko kudhani kuwa kapata janga njiani.

ROSS: Kutokuwepo kwake, bwana,
Kwafanya miadi aliyoiweka ilaumike.
Twaomba, bwana mtukufu, keti pamoja nasi.

MAKBETH: Meza imejaa.

LENOKSI: Hapa kuna kiti wakf, bwana.

MAKBETH: Wapi?

LENOKSI: Hapa, bwana mwema. Mbona washtuka, mtukufu?

MAKBETH (*akiona mzuka wa Banko na kudhani maiti imeketishwa pale*):
Ni nani, miongoni mwenu, kafanya hivi?

WAHESHIMIWA (*kwa mshangao*): Kitu gani, bwana wangu mwema?

MAKBETH (*akiusemesha mzuka wa Banko*):
Huwezi kusema ndimi niliyekutenda hivyo:
Usitikise kichwa chako kilichotapakaa
Damu mbele yangu.

ROSS: Waungwana, tuondoke; mfalme mtukufu
Ana kitu kinachomhofisha.

BIBI MAKBETH: Ketini, rafiki wastahiki: tabia yake
Hiyo si ngeni, bali kawaida toka ujana:
Tafadhali ketini; ana kipindu cha muda tu;
Kufumba na kufumbua, mtamwona ashekali.
Mkimkazia macho hivyo mtamchukiza,
Nacho kifafa kimsumbue kirefu zaidi.
Endeleeni kula, msijali hali yake.

(*Akimgeukia mumewe.*)

Wewe ni mwanamume, sivyo?

MAKBETH: Hakika, na ni dume shupavu, ninayethubutu
Kukiangaza kizushi kiwezacho kumtisha
Hata ibilisi halisi.

BIBI MAKBETH: O upuzi mtupu!
Hili ni jinamizi liletwalo na woga wako:
Hicho uogopacho ni mfano wa ile sime
Uliyosema uliiona imechomolewa

Hewani, na ambayo ulisema ilikuongoza
Chumbani mwa Dankan. O, kuhamanika hivyo!
Na sababu yake ni woga wa kujitendekeza,
Woga ambao wamfaa zaidi mwanamke
Anayesimulia hadithi itishayo mno,
Aketipo kando ya moto wakati wa kipupwe,
Na kujidai kuwa ukweli wa hadithi hiyo
Wathibitishwa na nyanya yake. Aibu kamili!
Mbona wafinya uso? Hakika hamna chochote,
Na bado wakikodolea macho kiti kitupu.

MAKBETH: Tafadhali, tazama pale! Angalia! Tazama!
Je, utaniambia hicho ni kitu gani basi?

(*Akiusemesha mzuka.*)

Najali nini, hata uwe mzuka wa Banko?
Watikisa kichwa, bila shaka waweza kunena.

(*Akisema mashavuni.*)

Kama makaburi na ahera vyahuisha wafu,
Basi, tumbo la mwewe liwe kaburi letu.

(*Mzuka unaondoka.*)

BIBI MAKBETH: Mbona wakosa heshima kwa mawazo ya upuzi?

MAKBETH: Ni yakini, niliposimama hapa, nilimwona.

BIBI MAKBETH: Kefule! Hiyo ni fedheha!

MAKBETH: Mauaji yamekuwapo tangu siku za kale,
Kabla sheria za kiungwana na maadili
Kuwapo na kuleta ustaarabu na wema;
Naam, na hata baada ya hapo mauaji
Yanayotisha na kusikitisha yametokea:
Mwanadamu, kwa jadi na asili, sharti afe
Kichwa kinapopasuliwa na ubongo kutapanywa,
Na hapo hufikia hatima ya maisha yake:
Lakini sasa wale waliokufa wafufuka,
Japo vichwani wana majeraha ishirini,
Na ambayo yanafisha, na kutunyang'anya viti:
Hii ni shani kubwa kuliko uuaji huo.

BIBI MAKBETH: Bwanangu mtukufu,
Rafiki zako waheshimiwa wanakungojea.

MAKBETH: Mara kwa mara ninasahau.
Rafiki wema, msiajabie tabia yangu;
Ninao udhaifu ambao si wa kawaida,
Usiowastaajabisha wale wanijuao.
Haya, natakia wote upendo na afya njema;
Baada ya kuwatakieni heri nitaketi:
Nipe divai, jaza kikombe changu farafara.
Nakunywa, nikitakia wote mezani shangwe,
Pia Banko, mpenzi wetu asiye hapa;
Na laiti angekuwa hapa! Ninyi nyote hapa,
Na Banko pia, nawatakieni heri nyote!

WAHESHIMIWA: Huduma yetu kwako, bwana, chini ya heri hiyo.

(*Unaingia tena Mzuka wa Banko.*)

MAKBETH: Ondokelea mbali! Hima, toweka usoni pangu!
Ardhi na ikufunike tena! Mifupa yako
Haina mafuta; damu yako ina ubaridi!
Macho ukodoayo hayakuonyeshi cho chote!

BIBI MAKBETH: Lifikirini jambo hili, waheshimiwa wema,
Kama udhaifu wa kawaida tu, si vingine;
Lakini unaiharibu karamu yetu.

MAKBETH: (*akiugombeza na kuuzomea mzuka wa Banko*):
Mimi mwanaume; siwezi kutishwa na mwingine:
Kama wapenda kunitaka shari, nikaribie
Kama dubu wa Urusi, mwenye singa za kimbimbi,
Au kama kifaru mwenye pembe inayotisha,
Au uje kama chui mkubwa wa Hirikana;
Au ujivike maumbile mengine yo yote—
Isipokuwa hali hiyo uliyo nayo sasa,
Nitasimama imara, na bila kutetemeka:
Au fufuka, tushindane kwa sime jangwani;
Nikiogopa kutoka, niite mwanasesere.
Ondokelea mbali, ewe kivuli uchukizaye!
Ewe maumbile ya dhihaka, ondokelea mbali!

(*Mzuka unaondoka.*)

Vema, ndivyo nipendavyo; kwa kuwa umetoweka,
Nimerudiwa na nafsi yangu ya kawaida.

(*Akiwageukia wageni.*)

Tafadhalini, kaeni kitako kwa utulivu.
BIBI MAKBETH: Umeichafua karamu hii; ukaharibu
Shangwe la jioni ya leo kwa makelele yako.
MAKBETH: Mambo kama haya yanapotokea kwa ghafula,
Kama mawingu ya kiangazi yatandavyo mbingu,
Inawezekanaje mtu asiyaajabie?
Mwanifanya hata niajabie tabia yangu,
Ninapoona ya kuwa ninyi mnavitazama
Vitu hivi kwa utulivu wenu wa kawaida,
Na ambapo mimi nimegeuka rangi kwa woga.
ROSS: Vitu gani, bwana wangu?
BIBI MAKBETH: Tafadhali, usimsemeshe; kwani hali yake
Itazidi kuwa mbaya; swali humghadhibisha.
Kwa hiyo ninawapeni buriani ya haraka:
Msikawie kupanga nani atoke kwanza,
Tokeni hobelahobela upesi muwezavyo.
LENOKSI: Kwa heri; namtakia mfalme afya njema!
BIBI MAKBETH: Nyote laleni unono!

(*Wote wanaondoka ila Makbeth na Bibi Makbeth.*)

MAKBETH: Sharti niadhibiwe kwa damu niliyomwaga;
Husemwa adhabu kwa mmwagaji damu ni damu:
Mauaji hayawezi kufichika; si ajabu
Mawe kutembea, miti kusema, na kufichua
Mauaji hayo; na mpiga ramli aweza,
Kwa kuchunguza dalili fulani azijuazo,
Na kuwasikiliza kunguru na ndege wengine,
Kugundua yule aliyemwaga damu kwa siri.
Yapata saa ngapi za usiku?
BIBI MAKBETH: Usiku umekomaa sana, na karibu kuche.
MAKBETH: Una maoni gani juu ya Makdaff kupuza
Mwaliko wetu na kutokuja kwenye shangwe hili?
BIBI MAKBETH: Je, ulimtumia habari, bwana?
MAKBETH: La, nimefahamu habari hiyo kwa bahati tu;
Lakini nitatuma: hamna, hata miongoni
Mwa waheshimiwa hawa, ambaye anayo nyumba
Isiyo na mtumishi niliyemwajiri mimi.
Kesho asubuhi na mapema nitawafuata
Wale Dada wa Ajali: wanieleze zaidi;
Kwani sasa natamani kufahamu sawasawa,

Na sijali kufuata uovu wa maovu!
Nitaviondosha vikwazo, nipate ufanisi:
Nimejitosa katika damu kiasi ambacho
Kurudi nyuma ni vigumu kama kusonga mbele.
Mawazo yangu yatishayo, yahitaji mkono;
Yatadhihirishwa kwa tendo kabla ya kupimwa.

BIBI MAKBETH: Wahitaji usingizi uburudishao mwili.

MAKBETH: Vema, twende tukalale. Maono yangu ya uongo
Yaletwa na woga wa kutokuzoea maovu,
Bado tu wanafunzi wa matendo ya uovu.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 5. Nyikani.

*Ngurumo. Wanaingia Wachawi watatu, wakakutana na* **Hekate.**

MCHAWI 1: Vipi; kuna shauri gani, Hekate!
Mbona umekasirika?

HEKATE: Nitakosaje kisa, kuwa na wachawi vikongwe,
Wenye utundu na ujuvi uletao hatari?
Mlithubutuje kushughulika na Makbeth,
Kwa mafumbo magumu, na mambo yaletayo kifo,
Na bila mimi, mungu wa uchawi na sihiri,
Niliye mfanya hila, na chanzo cha madhara,
Kuitwa nifanye sehemu yangu ilivyopasa,
Au niudhihirishe zaidi werevu wetu?
Tena, kosa lililo kubwa hata kuzidi hilo,
Ni kwamba vyote mlivyofanya mmemfanyia
Mtu mpotovu, atuchukiaye kwa ghadhabu;
Ambaye, kama watu wengine wote wafanyavyo,
Aonyesha mapenzi, apate muradi wake,
Lakini kumbe ninyi hawapendi hata kidogo.
Sasa rekebisheni makosa yenu: ondokeni;
Kesho asubuhi na mapema mkutane nami
Penye tundu la Acheron, lango la jehanamu:
Makbeth aja pale, ajue ajali yake:
Msisahau kutayarisha marigedi zenu,
Nyimbo za kunuizia uchawi, na mengineyo.
Sasa budi niruke hewani; na usiku huu,
Nitautafuta msiba unaotisha mno:

Kabla ya kesho adhuhuri, jambo kubwa mno
Litatekelezwa; kwenye pembe fulani ya mwezi
Pana tone la sihiri linaloning'inia!
Sina budi kuliwahi kabla ya kudondoka:
Na tone hilo likiisha chujwa kwa sihiri,
Litamfanya Makbeth awe katika njozi,
Kwa kuwa litamletea hali ya bumbuazi,
Na kumwingiza kwenye msiba wa maangamizi.
Hataogopa ajali, atadharau mauti;
Kupenda cheo kwake kutazidi hekima yake,
Na atapuza woga, na dhamiri inayomwonya:
Nanyi nyote mwajua kuwa kujiamini mno
Kwa mwanadamu, ni adui anayezidi wote.

(*Unasikilika Muziki na wimbo ndani.*)

Sikilizeni; Nimeitwa; hebu mtazameni
Mahoka wa Pepo kwenye ukungu akingojea.

(*Hekate anatoweka.*)

MCHAWI 1: Haya, twendeni haraka;
Hatakawia kurudi. (*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 6. Jumba la Mfalme. Forres.

*Wanaingia* **Lenoksi** *na Mheshimiwa mwingine.*

LENOKSI: Nilichokweleza, linganifu na mawazo yako;
Ni wajibu wako kufafanua maana hiyo:
Nasema kuwa mambo yameendeshwa kiajabu.
Yule Dankan adilifu alihurumiwa
Na Makbeth; ila, kwa jina la Mtakatifu
Mariamu, ilikuwa baada ya kifo chake:
Na Banko hodari katembea usiku mno;
Naye, unaweza kusema ikiwa unapenda,
Aliuawa na Flansi, kwani katoroka:
Kamwe haipasi watu kuchelewa nje usiku.
Ni nani awezaye kuliepuka wazo hili
Kwamba Malkom na Donalben walitenda
Uovu wa maovu kumwua baba yao mwema?
Naam, dhambi kubwa mno isiyoachilika!

Na kumbuka ilivyomhuzunisha Makbeth!
Je, hakuondoka hima kwa hasira adilifu,
Kuwararuararua wale wasiri wawili,
Walokuwa watumwa wa ulevi na usingizi?
Je, hilo si tendo la fadhila na heshima kubwa?
Hakika ndivyo; nalo lilikuwa tendo la busara,
Kwani ingemghadhibisha kila mwenye uhai,
Kuwasikia wakijikania jinaya hiyo.
Kwa hiyo, nakariri, alitenda ilivyopasa:
Na kama wale wana wa Dankan wangekuwa
Chini ya himaya yake, na Mungu apishe mbali,
Wangetambua thawabu ya kumwua baba yao;
Flansi, pia, angeona cha mtema kuni.
Sasa tunyamaze! kwani nimesikia tetesi,
Mfalme beberu kamwazirisha Makdaff,
Kwa kuwa alipuza mwaliko wake wa karamu,
Na kutoa siri nyingi kadamnasi ya watu:
Bwana, wafahamu anakosakini Makdaff?

MHESHIMIWA: Mwana wa Dankan,
Aliyepokonywa haki yake na beberu huyu,
Sasa kasakini katika jumba la mfalme
Wa Uingereza; na kapokelewa kwa huruma
Na mfalme Eduard aliye mtu sufii.
Ingawaje amekosa bahati ya ufalme,
Hajapungukiwa na chembe moja ya utukufu:
Makdaff amekwenda kumsihi mfalme
Huyo mtakatifu, kwa niaba ya Malkom,
Ashawishi Nothambalendi na Siwadi hodari
Kufanya vita. Kwa msaada wao na wa Mungu,
Tutaweza tena kula na kulala bila woga,
Tushereheke karamuni bila hofu ya kifo,
Tumtii mfalme wetu kwa uaminifu,
Atupe vyeo na heshima kwa njia ya halali;
Kwa sasa, mambo haya yote twayanolea meno.
Habari hizi zimemkasirisha Makbeth,
Hata anajaribu kujitayarisha kwa vita.

LENOKSI: Je, alimtuma mjumbe kumwita Makdaff?

MHESHIMIWA: Ndiyo: na Makdaff kasema "Bwana, kamwe siji,"

Na kwa ghadhabu yule mjumbe akarudi hima,

Huku akinung'unika kama kwamba alitaka
Kumwambia, 'Utalijutia mno jibu lako.'
LENOKSI: Na hili liwe onyo, ajitenge na Makbeth.
Laiti malaika mwema angemtangulia,
Aziwakilishe habari njema kwa mfalme
Kabla yake kuwasili huko Uingereza;
Na halafu nchi yetu iteswayo na beberu,
Iweze tena kujaliwa heri na neema!
MHESHIMIWA: Dua zangu na zifuatane naye safarini!
(*Wanaondoka.*)

## KITENDO CHA IV.

### Onyesho la 1. Kwenye pango. Katikati, marigedi inayochemka.

*Ngurumo. Wanaingia wale Wachawi watatu.*

MCHAWI 1: Mara tatu amelia,
Yule paka wa milia.
MCHAWI 2: Mara nne 'mesikia,
Nungunungu akilia.
MCHAWI 3: Hapia wangu kalia,
Sasa saa zawadia.
MCHAWI 1: Kuizunguka marigedi twendeni;
Matumbo yenye sumu ndani tupeni.
Chura aliyelala chini ya jiwe,
Siku thelathini na moja mwenyewe,
Na kurishai sumu nyingi mwilini,
Hapo alipolala usingizini,
Yeye achemshwe kwanza chunguni.
WOTE: Zidisha sana taabu na uchovu;
Moto waka na chungu kitoe povu.
MCHAWI 2: Kipande chembamba cha nyoka wa bwawa,
Kichemshwe, kikaangwe sawasawa;
Jino la kijusi cha huko ziwani,
Nacho kidole cha chura wa majini,
Manyoya ya popo, ulimi wa mbwa,
Ulimi kitao wa nyoka mkubwa,
Mwiba wa mdudu, guu la mjusi,

Na ubawa wa bundi, ili upesi
Mchanganyiko uletao makeke,
Ja mchuzi wa ahera uchemke.

WOTE: Zidisha sana taabu na uchovu;
Moto waka na chungu kitoe povu.

MCHAWI 3: Magamba ya nyoka, jino la mbwa mwitu,
Maiti ya mchawi ya mumiani,
Mzizi sumu ulochimbwa gizani,
Ongeza matumbo na koo la papa
Wa bahari chumvi, mla kwa pupa,
Ini la Myahudi asoamini,
Nyongo ya mbuzi mee tuimwage ndani,
Matawi ya mvinje yaliyokatwa
Wakati ambao mwezi umepatwa,
Pua ya Mturuki kafiri,
Na midomo ya Mtartari,
Kidole cha kitoto kilichonyongwa,
Ambacho kwenye handaki kilitupwa,
Na mamiye aliye mlaaniwa,
Muda mfupi tu tangu kuzaliwa:
Kwa mchuzi mzito kama ulimbo,
Ongeza ya chui mkubwa matumbo,
Mchanganyiko chunguni utimie.

WOTE: Zidisha sana taabu na uchovu;
Moto waka na chungu kitoe povu.

MCHAWI 2: Kwa damu ya nyani na tuupooze,
Kwa njia hiyo uganga tutimize.

*Anaingia* **Hekate**

HEKATE: O, vizuri sana! Nawasifu kwa juhudi zenu;
Kila mmoja 'tapata ijara kwa kazi yenu:
Na sasa izungukeni marigedi mkiimba,
Mithili ya pepo na vizimwi kwenye mduara,
Na mwekapo kitu cho chote katika marigedi,
Yabidi mwimbe wimbo wa kunuizia uchawi.

*Muziki na wimbo, "Pepo weusi," n.k.*

(*Hekate anatoweka.*)

MCHAWI 2: Vidole vyangu gumba vyawasha: hii
Yaonyesha aja mtu msafii.

Kufuli za mlangoni, fungukeni,
Huyo abishaye, mfungulieni!

*Anaingia* **Makbeth.**

MAKBETH: Vipi sasa, enyi wachawi, mnaokukurika
Usiku wa manane kwa siri! Mnafanya nini?

WOTE: Tendo lisilotajikana.

MAKBETH: Kwa jina la nguvu za sihiri na utabiri,
Ambazo mnazo, na sijali mnavyozipata,
Yajibuni maswali yangu: si kitu hata kama
Mtafungua kimbunga kiangushe mahekalu,
Au dhoruba ivunjayo na kuzamisha meli;
Hata mabua ya nafaka na miti iangushwe;
Nazo ngome ziwaangukie walinzi wake,
Na kuta za majumba ya wafalme na haram
Ziiname mpaka ziibusu misingi yake;
Hata kama mbegu za uhai zitaharibika,
Naam, hata uharibifu uone uchovu,
Yajibuni maswali nitakayowaulizeni.

MCHAWI 1: Sema.

MCHAWI 2: Uliza.

MCHAWI 3: Tutayajibu.

MCHAWI 1: Sema, utasikia majibu yetu,
Au ungependa ya wakubwa wetu?

MAKBETH: Waite, napenda kuwaona.

MCHAWI 1: Chunguni mwageni damu ya nguruwe,
Mla tisa, watoto wake mwenyewe;
Mafuta ambayo yatoka mtini,
Anyongwapo mwuaji, tupa motoni.

WOTE: Njoni wa vyeo vya juu na vya chini;
Sura na wajibu wenu onyesheni!

*Ngurumo. Mzuka wa* 1*: Kichwa chenye silaha.*

MAKBETH: Niambie, ewe pepo wa ajabu—

MCHAWI 1: Anayatambua mawazo yako:
Msikilize, fyata ulimi wako.

MZUKA 1: Makbeth, Makbeth, Makbeth, jihadhari
Na Makdaff!
Jihadhari na Sheki wa Fife. Nakwenda. Yatosha.

(*Mzuka unatoweka.*)

MAKBETH: Hata uwe nani, nakushukuru kwa onyo jema;
Umekigusa kiini cha woga moyoni mwangu:
Lakini naomba kuuliza kitu kimoja tu—

MCHAWI 1: Hakubali kulazimishwa: hapa yuko mwingine,
Na ambaye ana uwezo kuliko wa kwanza.

*Ngurumo. Mzuka wa 2. Mfano wa mtoto aliyetapakaa damu.*

MZUKA 2: Makbeth! Makbeth! Makbeth!

MAKBETH: Ningekuwa na masikio matatu,
Ningeweza kukusikia vizuri.

MZUKA 2: Nakutakia moyo wenye kutamani kuua,
Wenye ufidhuli na ugumu usobadilika;
Ubeze nguvu za wanadamu na kuwa mshari,
Kwa sababu hamna mzaliwa wa mwanamke
Awezaye kumdhuru Makbeth.

(*Mzuka unatoweka.*)

MAKBETH: Basi ishi, Makdaff: kwa nini nikuogope?
Walakini nitajihakikishia usalama,
Na Ajali itie muhuri: hivyo hutaishi;
Hatimaye niweze kuufariji moyo wangu,
Nibeze woga kama kitu kisicho na msingi,
Nilale fofofo hata zinapopiga ngurumo.

(*Ngurumo. Mzuka wa* 3. *Kitoto kilichoota mti kichwani.*)

Mzuka gani huu,
Unaojitutumua kama mwana mfalme,
Aliyevaa, katika kichwa chake cha kitoto,
Taji tukufu la kifalme?

WOTE: Msikilize, lakini usimsemeshe.

MZUKA 3: Nakutakia moyo kama wa simba, na kiburi;
Usimjali mtu anayekughadhibikia,
Wala wenye kulalama na kukufanyia hila:
Kamwe Makbeth hatashindwa mpaka msitu
Mkuu wa Benamu uamue kufanya hila,
Utakaposogelea mlima Dansinane.

(*Mzuka unatoweka.*)

MAKBETH: Jambo hilo haliwezi kutokea:
Mtu gani aweza kuutumikisha msitu,
Na kulazimisha miti ing'oe mizizi yake?
Huu ni utabiri upendezao sana! Vema!

Kwa hiyo ni kazi bure uasi kujitokeza
Kabla ya msitu wa Benamu kujihamisha;
Hivyo, kwa kuwa shani hiyo haiwezi kujiri,
Jabari Makbeth ataishi kwa usalama,
Hadi afe kwa mwujibu wa jadi ya binadamu.
Hata hivyo, moyo wangu bado watamani mno
Kulijua jambo moja: inawezekana kutokea
Watoto wa Banko watamalaki nchi hii?

WOTE: Usihitaji kufahamu zaidi.

MAKBETH: Ninapenda kupata jibu linalotosheleza:
Mkikataa, laana na iwe nanyi milele!
Nifahamisheni. Mbona chungu kinadidimia?
Na sauti hiyo yatoka wapi?

(*Matarumbeta.*)

MCHAWI 1: Jionyeshe!
MCHAWI 2: Jionyeshe!
MCHAWI 3: Jionyeshe!
WOTE: Jionyeshe machoni, uhuzunishe moyo wake;
Njoo kama kivuli, na utoweke vivyo hivyo!

(*Wanatokea Wafalme wanane, wa mwisho ana kioo cha usihiri mkononi; kisha Mzuka wa Banko unafuata.*)

MAKBETH: Washabihiana mno na mzuka wa Banko;
Ondokelea mbali!
Nawe, taji ulilovaa latia macho kiwi,
Na nywele zako zang'aa mno. Na wewe wa pili,
Mwenye taji kichwani, nywele ni kama wa kwanza:
Wa tatu kafanana na waliomtangulia.
Wachawi wakongwe! Kisa gani kunonyesha hayo?
Mfalme wa nne! Sipendi kuona zaidi!
Ajabu gani, msafara huu wa wafalme
Utaendelea hivyo hadi siku ya kiyama?
Bado mwingine! Na wa saba! Basi nafumba macho:
Tena bado atokea wa nane, mwenye kioo
Ambacho kinanionyesha wafalme zaidi;
Naona wengine mkono wa shoto wamebeba
Tufe mbili za dhahabu, na mkono wa kulia

Wakajibebesha fimbo tatu tatu za enzi:
Kizushi kinachotisha! Sasa naona ni kweli;
Mzuka wa Banko uliotapakaa damu
Unanichekelea kwa dhihaka na kunionyesha
Ya kuwa msafara huo ni wajukuu wake.

(*Mizuka inatoweka.*)

Nini, mambo haya yote yatajatokea hivyo?

MCHAWI 1: Ndiyo, bwana, vyote vitakuwa hivyo:
Mbona Makbeth aduwaa hivyo?
Dada, tumpe moyo achangamke,
Tumpe ukarimu akirimike;
Hewa nachawia, itoe muziki,
Nanyi zungukeni, kama kumlaki;
Na mfalme adhimu kwa huruma
Aweze kusema, wito wake mwema
Tumeuitikia na kulipia.

(*Muziki. Wachawi wanacheza, na kisha wanatoweka pamoja na Hekate.*)

MAKBETH: Wako wapi? Wametoweka? Saa hii ya uovu
Ikumbukwe katika takwimu saa laanifu!
Ingieni ndani, mngojao nje!

*Anaingia* **Lenoksi.**

LENOKSI: Wahitaji nini, mfalme mtukufu?

MAKBETH: Je, uliwaona wale Dada wa Ajali?

LENOKSI: Hapana, mfalme wangu.

MAKBETH: Hawakupita karibu nawe?

LENOKSI: Hakika hapana, mfalme wangu.

MAKBETH: Hewa wanayoipitia na iwawie sumu,
Nao wote walaaniwe wanaowaamini!
Nilisikia farasi: ulif'atana na nani?

LENOKSI: Ni wajumbe wawili ama watatu, bwana wangu,
Waliokuja kukuarifu kuwa Makdaff
Kakimbilia Uingereza.

MAKBETH: Kakimbilia Uingereza!

LENOKSI: Ndiyo, mtukufu wangu mwema.

MAKBETH: Wakati, wakimbia na kuzuia hila yangu;
Azimio kazi bure, kama hakuna matendo:

Tokea sasa, kila wazo linalotangulia,
Ni sharti mikono itangulie kulitenda.
Hata sasa, kuambatisha mawazo na matendo,
Yapasa azima na tendo kutokea pamoja:
Nitazingia ngome ya Makdaff kwa ghafula,
Nimtwalie mali na kukumba shamba la Fife;
Mkewe, vitoto vyake, na wote wa mbari yake,
Roho maskini, wataibusu ncha ya sime.
Kamwe sitajivuna kwa maneno kama mjinga:
Tendo nitalitenda kabla ya nia kupoa:
Walakini sipendi kuona mizuka zaidi!
Wajumbe hao wako wapi? Nipeleke waliko.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 2. Fife. Ngome ya Makdaff.

*Wanaingia* **Bibi Makdaff,** *Mwanawe, na* **Ross.**

BIBI MAKDAFF: Katenda nini kilichomfanya atoroke?
ROSS: Yakupasa kuwa na utulivu, bibie.
BIBI MAKDAFF: Hakuwa na kosa:
Kukimbia kwake kwaonyesha enda wazimu:
Woga hutufanya mahaini, hata bila tendo.
ROSS: Huelewi
Kama kakimbia kwa woga ama hekima yake.
BIBI MAKDAFF: Hekima! Kuacha mke, kuacha vitoto vyake,
Jumba lake na mali zake huku alikotoka?
Hatupendi; kapungukiwa mno na mapenzi:
Hata ndege mdogo kupita wote hupigana
Na bundi, kulinda makinda yake kwenye kiota.
Woga wake unaelemeza mapenzi yake;
Hekima yake ni ndogo, kakimbia bila kisa.
ROSS: Binamu yangu mpenzi,
Nakusihi utulie: usimhofie mumeo,
Kwani yu mtukufu, mwenye hekima na busara,
Mwenye kuzitambua rabsha za nyakati hizi.
Sitathubutu kuzungumza zaidi sasa:
Ila nasema nyakati hizi zimerabishika,
Ambapo twaitwa mahaini, bila kujijua,
Na kuuamini uvumi kwa ajili ya woga,

Hata tusipojua ni jambo gani twaogopa,
Twaelea katika hofu na woga kama chombo
Kinojisukasuka kwenye bahari ya dhoruba.
Nakuacha sasa: sitakawia kurudi tena:
Uovu ufikiapo upeo wake hukoma,
Au mambo hurudia hali yake ya mwanzo.
Binamu mpendwa, nakutakia kila la heri!

BIBI MAKDAFF: (*akimgeukia mwanawe*):
Kapata kuwa na baba, bali sasa hana baba.

ROSS: Nitakuwa mjinga mno nikikawia hapa,
Nitajifedhehesha, nikuzidishie huzuni:
Nakuaga niondoke hima. (*Anaondoka.*)

BIBI MAKDAFF: Maskini mwanangu, babiyo kafa;
Utatenda jambo gani sasa? Na utaishije?

MTOTO: Nitaishi kama ndege, mama.

BIBI MAKDAFF: Nini, waweza kuishi kwa wadudu na nzi?

MTOTO: Kwa cho chote nipatacho; ndivyo nao wafanyavyo.

BIBI MAKDAFF: Kinda maskini! Usingaliogopa hatari,
Ya wavu, wala ulimbo; wala rima na mtego.

MTOTO: Niogope nini, mama? Ndege duni hawategwi.
Lakini babangu hajafa, hata useme nini.

BIBI MAKDAFF: Yakini, amekufa: utaishije bila baba?

MTOTO: La; je, wewe utaishije bila kuwa na mume?

BIBI MAKDAFF: Kwa nini, naweza kujinunulia ishirini,
Katika soko lo lote.

MTOTO: Basi utawanunua makusudi uwauze.

BIBI MAKDAFF: Wasema kwa akili ya ucheshi unavyoweza,
Na hakika, hiyo ni akili inayokutosha.

MTOTO: Je, baba yangu alikuwa haini, mama?

BIBI MAKDAFF: Hakika, ndivyo.

MTOTO: Haini ni mtu wa namna gani?

BIBI MAKDAFF: Ha, ni mtu anayeapa, na kisha kuongopa.

MTOTO: Je, wote wafanyao hivyo huitwa mahaini?

BIBI MAKDAFF: Kila mmoja afanyaye hivyo ni haini, naye
Sharti anyongwe.

MTOTO: Na italazimu wote wanaoapa
Kisha kuongopa wanyongwe?

BIBI MAKDAFF: Kila mmoja.

MTOTO: Nani itambidi kuwanyonga?

BIBI MAKDAFF: Aha, mtu aliye mwaminifu.
MTOTO: Basi watu waongo na wenye kuapa yamini
Ni wajinga, kwani kuna waongo na waapizi
Wanaotosha kuwapiga watu waaminifu,
Na halafu kuwanyonga wote.
BIBI MAKDAFF: Basi, kitoto kitundu, Mungu akusaidie!
Lakini utaishije bila baba?
MTOTO: Kama ingekuwa amekufa, ungeomboleza:
Na kama hungeomboleza, basi, ingalikuwa
Ishara ya tumaini kupata baba mwingine.
BIBI MAKDAFF: Maskini mpayupayu, wabwabwaja, naam!

*Anaingia Mjumbe*

MJUMBE: Salamu, bibie mwema! Hakika hunifahamu,
Ila mimi natambua hadhi na heshima yako.
Ninashuku kuna hatari inayokunyatia:
Ikiwa utalisikiza onyo la mtu duni,
Ni heri usikutwe hapa; ondoka na wanao.
Kukuogofya hivyo, natambua ni ukatili,
Lakini kama ningeacha kukupa onyo hilo,
Ingekuwa ukatili kama unaonyatia
Kuudhuru mwili wako. Mungu na akuhifadhi!
Sithubutu kukawia hapa zaidi.

(*Anaondoka.*)

BIBI MAKDAFF: Nitakimbilia wapi?
Sijatenda udhalimu. Ila sasa natambua,
Naishi katika ulimwengu huu wenye dhambi;
Ambako kufanya madhara, aghalabu, ni sifa,
Na kutenda mema, mara nyingine, niupumbavu:
Basi, maskini, mbona nakinga nafsi yangu
Kwa ukakamavu wa mwanamke, nikitetea
Kwamba sijatenda udhalimu?

*Wanaingia Wauaji.*

Nyuso gani hizi?
MWUAJI 1: Mumeo yuko wapi?
BIBI MAKDAFF: Natumaini, hayupo mahali penye najisi,
Ambapo washari kama ninyi waweza kumwona
MWUAJI 1: Yeye ni haini.
MTOTO: Waongopa, ewe mshari mwenye nywele kimbimbi!

MWUAJI 1: Wasema nini, ewe yai?
Mbegu changa ya uhaini!

(*Akimchoma sime.*)

MTOTO: Ameniua, mama:
Tafadhali kimbia!

(*Anakufa.*)

*Anatoka Bibi Makdaff akilia, 'Mauaji'! wanatoka Wauaji wakimfuata.*

**Onyesho la 3. Uingereza. Mbele ya jumba la mfalme.**

*Wanaingia* **Malkom** *na* **Makdaff.**

MALKOM: Twende zetu faraghani, mahali penye kivuli,
Hapo tuomboleze, machozi yatakase moyo.
MAKDAFF: Heri tusimame kwa uthabiti na sime zetu,
Na kama watu wema, tupiganie nchi yetu,
Ambayo yalemezwa na msiba: mapambazuko
Ya kila siku, wajane wapya kupiga mayowe,
Yatima wapya kulia, maafa mapya kusibu—
Sauti za huzuni zikaielekea mbingu,
Ambayo yaelekea, kwa kutoa mwangwi wake,
Kuwa inaihurumia nchi ya Skotia,
Inaporudisha sauti hiyo yenye huzuni.
MALKOM: Kwa kile ninachokiamini, nitaomboleza,
Na kile ninachokifahamu, nitakiamini,
Na cho chote ambacho naweza kukirekebisha,
'Kipata wasaa ufaao, nitarekebisha.
Mambo uliyoyasema, yumkini, ni ya kweli.
Beberu huyo, mwenye jina lituchomalo ndimi,
Alipata kudhaniwa kuwa mtu mwaminifu:
Na wewe umepata kumpenda kwa moyo wote;
Naye hajapata kukudhuru. Mimi ni kijana:
Huenda watazamia tuzo kwa kunisaliti,
Na hakika, ni jambo la busara kutambikia
Mwana kondoo, maskini, asiye na hatia,
Ili kumtuliza mungu aloghadhibika.
MAKDAFF: Mimi si msaliti.
MALKOM: Lakini Makbeth ni msaliti:
Hata mtu mwema na mwenye nasaba adilifu,
Aweza badilika kwa amri ya mfalme.

Walakini nisamehe kwa kukutilia shaka;
Mashaka niliyo nayo hayawezi kubadili
Tabia yako ya jadi: malaika watang'aa,
Ingawaje yule aliyeng'aa kuliko wote
Alimkosea Mungu. Na hata uovu wote
Ukijisetiri katika joho la maadili,
Sharti maadili halisi yatambulikane.

MAKDAFF: Nimekata tamaa.

MALKOM: Labda ni kwa sababu nilikutilia shaka.
Kitu gani kilikufanya uharakishe kuja,
Kwa hamaki ukatelekeza mke na watoto,
Walio tunu zivutazo, shina la mapenzi,
Bila kuwaaga? Kunradhi, usidhani kuwa
Nimekutilia shaka kukuvunjia heshima,
Bali napenda kujihakikishia usalama.
Yawezekana kuwa wewe u mtu adilifu,
Hata kama nitakudhania kuwa u vingine.

MAKDAFF: Basi, nchi yangu, endelea kutokwa na damu!
Beberu, waweza kuimarisha msingi wako,
Kwani wema waogopa kupinga uovu wako:
Jifaharishe na matunda ya udhalimu wako;
Cheo ulichojipa kimekukaa barabara!
Nakupa kwaheri, bwana: sipendi kuwa haini,
Unavyonidhania, hata nikipewa milki
Yote ambayo ameifumbata beberu huyo,
Na hata niongezewe Mashariki ya neema.

MALKOM: Usikasirike:
Kukuogopa, sicho kisa chote kusema hayo.
Ninadhani nchi yetu inazama utumwani;
Inaomboleza, yatoka damu, na kila siku
Jeraha jipya laongeza idadi ya madonda:
Natumai pia, wengi wataniunga mkono,
Katika kupigania urithi wangu; na hapa,
Mfalme wetu mtukufu wa Uingereza,
Kaniagia maelfu ya askari bora:
Walakini hata nikifanikiwa, naogopa,
Hapo nikiisha kata kichwa cha beberu huyo,
Na kukanyaga juu yake, au kukichomeka
Kwenye ncha ya sime yangu, huenda maskini
Nchi yangu itapata maovu mengi zaidi;

Itateseka kwa njia nyingi isizozijua,
Chini ya mfalme atakayefuata.

MAKDAFF: Atakuwa mtu wa namna gani?

MALKOM: Yaani ni mimi mwenyewe, ambaye najijua:
Nina jadi ya kupenda maovu kila aina,
Na ambayo yatakaponikolea barabara,
Makbeth mweusi ataonekana mweupe,
Mfano theluji, na maskini taifa letu,
Limstahi astahilivyo mwana-kondoo,
Wanapomlinganisha na dhuluma yangu kubwa.

MAKDAFF: Hata miongoni mwa vikosi
Vya ibilisi wa jehanamu, hamna ye yote
Awezaye kumzidi Makbeth kwa uovu.

MALKOM: Nakubali ya kuwa yu mkatili kiuaji,
Mshaufu, batili, mdanganyifu, mlaghai,
Mgomvi, habithi, na kwa kifupi ana chembe
Ya kila dhambi iliyopata kutajwa po pote:
Lakini ashiki yangu nyingi haina kipimo:
Na anasa yangu yaelemeza vipingamizi—
Vyote vinavyojaribu kupinga tamaa yangu:
Heri Makbeth, kuliko mwenye tabia hiyo,
Kutawala.

MAKDAFF: Kukosa tawasufi, kwa asili ni ubeberu;
Ndiyo chanzo cha kuuzuliwa kwa wafalme,
Na kukabiliwa na mauti yao kwa ghafula.
Walakini usiogope kudai haki yako:
Unaweza kuishi katika anasa kwa siri,
Na hadharani uonekane mwenye tawasufi.

MALKOM: Pamoja na hayo, nina tabia nyingine mbaya;
Ninayo tamaa ya mali isiyotosheleka,
Na kama' ngalikuwa mfalme, ningewanyonga
Masharifu wote ili nikumbe makonde yao,
Kisha huyu nimpokonye johari, yule nyumba:
Na kupata vitu hivi, kutakuwa kishawishi,
Kizidishe tamaa yangu ya kupata zaidi;
Kwa hiyo ningezua ugomvi pasipo haki,
Niwashtaki raia wema na waaminifu,
Mradi niwaangamize, nikumbe mali zao.

MAKDAFF: Tamaa hiyo ya mali
Hukolea zaidi, na mizizi yake mibaya,

Hudumu kuliko ile ya ashiki ipitayo,
Na imekuwa sime, kuchinja wafalme wetu:
Lakini, hata hivyo, usiogope; Skotia
Inayo mali isiyopimika; nayo ni yako,
Waweza kuitumia hata ujitosheleze:
Chembe hizo zote za uovu zinavumilika,
Kama tukizilinganisha na utukufu wako.

MALKOM: Lakini sina utukufu: sifa za kifalme
Kama haki, uaminifu, kiasi, utulivu,
Ukarimu, uthabiti, huruma, unyenyekevu,
Uchaji, uvumilivu, uhodari, ushupavu,
Sina hata harufu yake; lakini ndani mwangu
Mna uovu wa aina kadha kwa njia nyingi.
La, ningalikuwa na mamlaka, ningebadili
Amani yetu tamu kama maziwa kuwa chuki
Ya jehanamu; nipangue mapatano ya watu,
Nivunje njia zote za umoja ulimwenguni.

MAKDAFF: O Skotia, Skotia!

MALKOM: Kama mtu wa sifa hizo aweza kutawala,
Niambie: nina tabia niliyokueleza.

MAKDAFF: Aweza kutawala!
La, hawezi kuishi. O taifa lenye taabu,
Lenye beberu ashikaye mamlaka kwa nguvu,
Na mwenye fimbo yenye damu itoayo mvuke;
Lini utarudiwa na afya yako ya zamani,
Ambapo mrithi halisi wa kiti cha enzi,
Kashtakiwa na dhamiriye na kujilaani,
Na hivyo kawachongea wote wa ukoo wake?
Baba yako mtukufu alikuwa mfalme
Adilifu kuliko wote: malkia, mamiyo,
Aghalabu alipiga magoti akijirudi,
Na maisha yake yakawa kama ya kujitesa.
Nakupa kwa heri! Maovu hayo unojivika
Yamenifukuza nyumbani Skotia. O moyo
Wangu, matumaini yako yote yakoma hapa!

MALKOM: Makdaff, hiyo huzuni yako ya utukufu,
Na ambayo yatokana na uadilifu wako,
'Meniondolea mashaka yote moyoni mwangu,
Na imenihakikishia wema, uaminifu,
Na hadhi yako. Makbeth mwovu amejaribu,

Kwa njia nyingi kama hizo, kunitia nguvuni;
Na dhamiri yanionya, nisiamini kijinga:
Lakini Mungu aamue kati yangu na yako!
Kwani tangu sasa nategemea wongozi wako,
Na nioshe lawama lote nililojitwisha;
Mbele yako najikania athari ya uovu,
Na lawama nililojipa sasa hivi mwenyewe,
Kwani uovu wa aina yo yote siujui.
Sijaujua uke, sijashuhudia uongo,
Sijapata kutamani mali, hata iwe yangu,
Sijapata kuvunja ahadi yangu kwa ye yote,
Simsaliti ibilisi, hata kwa mwenzake,
Nami nathamini ukweli kama maisha yangu:
Mara yangu ya kwanza kushuhudia uongo,
Ni hapa, nilipojishuhudia mimi mwenyewe:
Kwa kuwa nimekweleza tabia ya moyo wangu,
Nangoja amri kutoka kwako na nchi yangu:
Kabla yako kufika hapa, mzee Siwadi,
Pamoja na askari hodari elfu kumi,
Walikwisha kujitayarisha kupigana vita.
Sasa kwa kuwa umekuja tuondoke pamoja;
Tufanikiwe vema, nia yetu ilivyo njema!
Mbona wanyamaza kimya?

MAKDAFF: Mambo hayo yafurahishayo na kuhuzunisha,
Kwa mara moja, ni vigumu kuyaafikanisha.

*Anaingia Daktari Mskotia.*

MALKOM: Vema; tutazungumza zaidi baadaye. Je,
Mfalme atatoka nje hivi karibuni?

DAKTARI: Ndiyo, bwana; umati mkubwa wa watu dhalili
Wangojea awaguse na kuwaponya maradhi;
Maradhi yao yaelemeza utabibu wote:
Ila mkono wake Mungu kauweka wakf—
Naye akiwagusa wapona mara hiyo hiyo.

MALKOM: Nakushukuru, Daktari.

(*Daktari anaondoka.*)

MAKDAFF: Anasema huo ni ugonjwa gani?

MALKOM: Huitwa maradhi ya mti:
Mfalme huyu mwema hufanya mambo ya shani;

Aghalabu, tangu nifike hapa Uingereza,
Nimeshuhudia akifanya miujiza hiyo.
Awezavyo kumshawishi Mungu kwa sala zake,
Mwenyewe ajua: ila wagonjwa wa kipekee,
Waliovimba tezi na wenye banguzi, naam,
Wanohuzunisha macho na kushinda utabibu,
Yeye huwaponya, anapowavalisha sarafu
Ya dhahabu shingoni, akiomba dua takata:
Yasemekana kuwa atamrithisha mrithi
Wa kiti cha enzi kipawa chake cha kuponya.
Mbali na kipawa hicho cha ajabu cha kuponya,
Mungu amemjalia kipawa cha utabiri,
Na baraka nyingi zazunguka kiti cha enzi,
'Kimtangaza kama mbarikiwa mteule.

*Anaingia* **Ross.**

MAKDAFF: Hebu tazama, nani anakuja hapo?
MALKOM: Mwananchi mwenzangu; ila sijamtambua.
MAKDAFF: Binamu yangu mwungwana, twakukaribisha hapa.
MALKOM: Sasa namtambua: namwomba Mungu aondoe
Kile kipingamizi kinachotenga wananchi!
ROSS: Bwana, Amina.
MAKDAFF: Je, huko Skotia mambo yako yalivyokuwa?
ROSS: Maskini, nchi yangu,
Karibu iogope kutambua nafsi yake!
Haipasi kuitwa mama bali kaburi letu:
Hamna anayetabasamu, hata mara moja,
Labda ni msungo, asiyejua cho chote;
Kite, maumivu, na yowe husikika hewani,
Navyo ni kawaida asiyoijali ye yote;
Naam, majonzi ni harara ya kawaida:
Kengele za kifo husikika, lakini hamna
Wa kuuliza nani kafa; na wengi wenye afya
Hufa kabla ya maua kwenye kofia zao
Kunyauka, na hata kabla yao kuugua.
MAKDAFF: O, maelezo kamili, yenye ukweli mtupu!
MALKOM: Kuna majonzi gani ya hivi karibuni?
ROSS: Hayo ya saa moja iliyopita ni ya kale,
Na sharti mwelezaji ayafanyie mzaha,
Kwa kuwa kila dakika huleta huzuni mpya.

MAKDAFF: Mke wangu yu hali gani?
ROSS: Nzuri tu.
MAKDAFF: Na watoto wangu wote?
ROSS: Wao, pia.
MAKDAFF: Yule beberu hajawatia msukosuko?
ROSS: La; nilipowaacha, walikuwa na amani.
MAKDAFF: Usibanie maneno; mambo yakoje?
ROSS: Nilipokuwa nikija hapa kuleta habari,
Na ambazo zimeulemea mno moyo wangu,
'Lisikia tetesi, wengi jasiri wameasi;
Nami binafsi nikashuhudia askari
Wa yule mfalme mdhalimu katika mwendo:
Sasa ni wakati wa kusaidia nchi yako;
Kuwepo kwako Skotia, 'tatupa askari,
Na hata kutawafanya wanawake wapigane,
Wajiondolee kibuhuti kinachowatisha.
MALKOM: Waburudike,
Tunakuja huko: hapa mtukufu mfalme
Wa Uingereza katupa jemadari Siwadi,
Pamoja na askari hodari elfu kumi;
Kamwe hakuna jemadari hodari kama yeye,
Katika nchi zote zenye dini ya Kikristo.
ROSS: Laiti ningekuwa na jibu lenye kuliwaza,
Kama maneno hayo yanayoburudisha moyo!
Lakini habari nilizo nazo zastahili
Kusemwa jangwani pasipo mtu wa kusikia.
MAKDAFF: Zamhusu nani?
Watu wote? Au mtu mmoja tu binafsi?
ROSS: Hamna ye yote mnyofu asiyesikitika;
Lakini hasa zinakuhusu wewe binafsi.
MAKDAFF: Kama zanihusu mimi,
Usinifiche; nieleze vyote kinaganaga.
ROSS: Basi sikio lako lisiichukie sauti
Ya ulimi wangu milele, litakaposikia
Jambo chungu kuliko lililopata kusikia.
MAKDAFF: Ha! Naweza kukisia unachotaka kusema.
ROSS: Ngome yako imeshambuliwa ghafula: mkeo,
Na watoto wako wakachinjwa kikatili mno:
Kama nikieleza jinsi walivyouawa,
Nitajumlisha kifo chako katika orodha

Ya hao walouawa kama paa maskini.

MALKOM: Mungu mwenye huruma!
Jipe moyo, mwanamume! Usiivute kofia,
Kulifunika paji la uso; yape majonzi
Maneno: ghamu isiyojitokeza kwa maneno,
Hunong'oneza moyo uliojaa majonzi,
Na hutafuta kuupasua.

MAKDAFF: Watoto wangu pia?

ROSS: Mkeo, watoto, watumishi, wote
Walioweza kuonekana.

MAKDAFF: Nami sikuwepo huko!
Mke wangu kauawa pia?

ROSS: Nimekwambia.

MALKOM: Jipe moyo:
Basi na tuyafanye malipizi kuwa mapoza,
Kuponyesha majonzi haya yaliyo mazito.

MAKDAFF: Hana watoto. Kaviua vitoto vyangu vyote?
Je, ulisema vyote? O mwovu gani! Wote? nini,
Vifaranga vyangu vyanana vyote, na mama yao,
Kaviangusha kikatili mkupuo mmoja?

MALKOM: Shindana na majonzi yako kama mwanamume.

MAKDAFF: Nitafanya hivyo;
Lakini sharti nisikitike kibinadamu.
Sitasahau kuwa nilikuwa na watu hao,
Na ya kuwa niliwathamini mno maishani.
Mungu alishuhudia, na bila kusaidia?
Makdaff mkosaji, dhambi zangu 'mewaua!
Mimi ni kiumbe kisicho na faida yo yote,
Wameuawa kwa makosa yangu, wala si yao.
Mungu na awape malazi mema!

MALKOM: Majuto hayo yawe ni kinoo cha sime yako:
Yabadilishe majonzi yako kuwa hasira;
Usifanye moyo butu, chochea harara yake.

MAKDAFF: Laiti ningeweza kulia kama mwanamke,
Na kujigamba kwa ulimi! Lakini, Mungu mwema,
Ondoshelea mbali vipingamizi; uso kwa uso
Nimkabili huyo ibilisi wa Skotia;
Mlete karibu na sime yangu; akitoroka,
Mungu msamehe kama nitakavyomsamehe!

MALKOM: Hayo ni maneno ya kiume,

Haya, twende kwa mfalme; jeshi letu tayari;
Kilichobakia sasa ni kumwaga mfalme;
Wakati wa kumtingisha Makbeth ni huu,
Na nguvu za mbinguni zituchochee, sime zao.
Jipe moyo: hakuna refu lisilo na mwisho.

(*Wote wanaondoka.*)

## KITENDO CHA V

### Onyesho la 1. Dansinane. Ukumbi kwenye ngome ya Makbeth

*Wanaingia Daktari Mwingereza na Mwanamke mwungwana.*

DAKTARI: Nimekesha pamoja nawe siku mbili, lakini sijaona ukweli wa taarifa yako. Lini katembea usingizini mara ya mwisho?

MWANAMKE: Tangu mfalme mtukufu alipoanza vita, nimemwona malkia akiamka, akavaa joho lake la kulala, akafungua kisanduku chake, akachukua karatasi, akaikunja, akaandika juu yake, akaisoma, na kisha akaifunga na kurejea kitandani tena; na wakati wote huu huwa kalala fofofo.

DAKTARI: Ana udhaifu mkubwa mwilini, kuweza kupata kwa pamoja baraka ya usingizi na kutimiza matendo yatendwayo na asiyelala! Katika usingizi wake, na kuachilia mbali kutembea kwake na matendo yake ya usingizini, umemsikia akisema lo lote?

MWANAMKE: Ndiyo, bwana; ila ni jambo ambalo kwalo sitamsengenya.

DAKTARI: Waweza kunieleza mimi; na yapasa sana unieleze.

MWANAMKE: Sitakueleza wewe wala mwingine ye yote; kwani sina shahidi wa kuthibitisha kile nitakachosema.

*Anaingia* **Bibi Makbeth** *akiwa na mshumaa.*

Tazama, huyu anakuja mbele yetu! Hivyo ndivyo afanyavyo kila mara; na, naapa, yu usingizini kabisa. Mchunguze vema; simama kifichoni umchunguze.

DAKTARI: Kapataje mshumaa unaowaka?

MWANAMKE: Ulikuwa karibu na kitanda chake; ni kwamba hupendelea kuwa na mshumaa unaowaka kucha; katoa amri hiyo.

DAKTARI: Unaona, macho yake yanaangaza.

MWANAMKE: Kweli; lakini hayaoni cho chote.

DAKTARI: Anafanya nini sasa? Tazama anavyosugua mikono yake.

MWANAMKE: Hiyo ni kawaida yake; huonekana kama kwamba ananawa mikono: nimepata kumwona akiendelea hivyo kwa robo saa.

BIBI MAKBETH: Hata hivyo, bado limebakia doa.

DAKTARI: Sikiliza! Anasema: nitaandika atakachosema ili niweze kujikumbusha baadaye.

BIBI MAKBETH: Yeyuka, doa maluuni! Yeyuka, nakuamuru! Moja, mbili; basi huu ndio wakati wa kulitenda tendo hilo.—Jehanamu kuna giza!—Kefule, bwanangu, kefule! Wewe ni askari na bado unaogopa? Tuna haja gani kumwogopa ye yote atakayejua iwapo hamna wa kutulazimisha tueleze kisa cha matendo yetu?—Lakini nani angeweza kudhani mzee yule alikuwa na damu nyingi kiasi hicho?

DAKTARI: Umezingatia alichosema?

BIBI MAKBETH: Sheki wa Fife alikuwa na mke: mkewe yuko wapi sasa?—Nini, mikono hii haiwezi kutakata kamwe?—Basi yatosha, mume wangu, yatosha: unaliharibu shangwe lote basi kwa kushtukashtuka hivyo.

DAKTARI: Kefule, kefule; umelifahamu jambo ambalo haikukupasa kulifahamu.

MWANAMKE: Amesema jambo ambalo haikumpasa kulisema, nina hakika; lakini hilo jambo alilofahamu, Mungu pekee alijua.

BIBI MAKBETH: Hapa bado pana harufu ya damu: manukato yote ya Manga hayawezi kukipa kikono changu hiki harufu nzuri. Oh, oh, oh!

DAKTARI: Anahema kiasi gani! Moyo wake umejaa huzuni ya majuto.

MWANAMKE: Singetamani kuwa na moyo kama wake; hata kama ningeahidiwa fahari ya utu wake.

DAKTARI: Kuna salama hapa?

MWANAMKE: Mwombe Mungu ajalie hivyo, bwana.

DAKTARI: Ugonjwa huu washinda ujuzi wangu: lakini nimepata kuwaona watembeao usingizini, ambao waliendelea kuishi vema hadi wakafa kwa amani vitandani mwao.

BIBI MAKBETH: Nawa mikono, vaa joho lako la kulala; usijifishe hivyo.—Nakwambia hata mara nyingine tena, Banko amekwisha zikwa; hawezi kutoka kaburini.

DAKTARI: Mna simanzi hiyo pia?

BIBI MAKBETH: Twende zetu kitandani, twende! Kuna agongaye mlangoni: njoo, njoo, njoo, njoo, nipe mkono wako; kilichotendeka kimetendeka. Kitandani, kitandani, kitandani.

(*Anaondoka.*)

DAKTARI: Atakwenda kitandani sasa?

MWANAMKE: Moja kwa moja.

DAKTARI: Hewa imejaa uvumi mbaya: matendo yasiyo
Ya kawaida, hufuatwa na maradhi yasiyo
Ya kawaida: dhamiri zenye hatia huficha
Siri, ila huinong'oneza mito yao bubu:
Anahitaji kasisi hata kuliko tabibu.
Mungu, Mungu tusamehe sote! Mtunze vema;
Mlinde na kumwepusha madhara yote ya mwili,
Na kila mara ukumbuke kumkazia macho.
Basi, buriani: kaelemeza akili zangu,
Na kunipumbaza kabisa nilipomtazama.
Nawaza mengi, lakini sithubutu kuyasema.

MWANAMKE: Buriani, Daktari mwema.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho 2. Mbugani karibu na Dansinane

*Ngoma na beramu. Wanaingia* **Menteth, Kathne, Angasi, Lenoksi,** *na Askari.*

MENTETH: Jeshi toka Uingereza lakaribia kuja,
Nalo laongozwa na Malkom, mjomba wake
Siwadi, na Makdaff mwema: kulipa kisasi,
Ndiyo kichocheo chao; na kusudi lao jema

Litamfanya hata yule asiye na harara
Asisimke, apigane vita vyenye kutisha.

ANGASI: Pale karibu na msitu Benamu
Tutakutana nao; watakuja kwa njia hiyo.

KATHNE: Je, kuna anayefahamu kama Donalben
Kafuatana na kaka yake?

LENOKSI: Kwa kweli, bwana, hayupo naye; ninayo orodha
Ya waungwana wote: ila yuko mwana Siwadi,
Pamoja na ghulamu wengi wasioota ndevu,
Wakidhihirisha, kwa awali, moyo wa kiume.

MENTETH: Beberu Makbeth anafanya nini?

KATHNE: Anailinda ngome yake huko Dansinane;
Watu fulani fulani wasema ana kichaa:
Na wengine, wasiomchukia kiasi hicho,
Watetea kuwa ana ghadhabu ya kishujaa:
Lakini, kusema kweli, hataweza kutiisha
Jeshi lake shaghala baghala lif'ate amri.

ANGASI: Sasa ndipo asikia
Mauaji yake ya siri 'kinata mikononi;
Kila dakika sasa uasi mpya watokea,
Na kumkaripia kwa uhaini alofanya;
Wanomfuata ni kwa amri, si mapenzi:
Na sasa anasikia cheo alichojivika
Chalegalega kama joho la mtu pandikizi
Linavyolegalega mwilini mwa mtu kibeti.

MENTETH: Basi nani atamlaumu,
Akili zikimruka kwa kuhamanika mno,
Na wakati ambapo vyote vilivyo ndani yake,
Vitajilaumu vikijutia kuwemo humo?

KATHNE: Haya, tufunge safari,
Twendeni kumtii yule anayestahili:
Tukutane naye, ndiye dawa ya taifa gonjwa;
Na tukiungana naye, tuokoe nchi yetu,
Tukiitakasa kwa kila tone la damu yetu.

LENOKSI: Au kiasi cho chote kitakachohitajika;
Damu yetu imhuishe mfalme wa haki,
Kama umande unavyolihuisha ua zuri,
Na kisha kuyazamisha magugu ya ubeberu.
Tufunge safari kuelekea Benamu.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 3. Dansinane. Chumba katika ngome ya Makbeth

*Wanaingia* **Makbeth,** *Daktari, na Wahudumu.*

MAKBETH: Usinipe taarifa zaidi; waende wote:
Kabla ya msitu wa Benamu kujiondosha
Mahali pake na kusogelea Dansinane,
Sitaweza kuwa hata na chembe moja ya woga.
Hicho kitoto, Malkom, ni nani? Kazaliwa,
Ama hakuzaliwa na mwanamke? Zile pepo,
Zijuazo vyote vimtokeavyo mwanadamu,
Zilinambia hivi, "Usiogope, Makbeth;
Hamna ye yote alozaliwa na mwanamke,
Atakayeweza kupata ushindi juu yako."
Basi, nitorokeni, enyi masheki wanafiki,
Jiungeni na wapenda anasa Waingereza:
Akili zinazoniongoza, na moyo hodari,
Kamwe havitalemewa na mashaka wala woga.

*Anaingia Mtumishi.*

Ibilisi mwovu na akupake rangi nyeusi,
Ewe kitwana uliyechujika rangi usoni!
Mbona waonekana kama bata aliyetishwa?

MTUMISHI: Kuna elfu kumi—

MAKBETH: Mabata, kitwana?

MTUMISHI: Askari, bwana.

MAKBETH: Nenda jitoboe uso, damu ifunike woga,
Ewe kitwana kinyonge. Askari gani, bunga?
Maleuni na roho yako! Hayo mashavu yako
Yaliyogeuka rangi ni kishawishi cha woga.
Askari gani, mwoga ulofifia rangi?

MTUMISHI: Jeshi la Kiingereza, mfalme mtukufu.

MAKBETH: Ondosha uso wako mbele yangu.

(*Mtumishi anaondoka.*)

Seyton! Moyo wangu ni mzito kwa huzuni,
Ninapoona—Seyton, je, wanisikiliza?
Shambulio hili ama litaniimarishia
Kiti cha enzi, ama sasa litaninyang'anya.
Nimeishi kirefu cha kutosha: maisha yangu
Yanapukutika kama majani ya kimanjano;

Na sifa njema zinazoambatanana uzee,
Kama heshima, mapenzi, utiifu, kikundi
Cha marafiki, sitategemea kuzipata;
Walaki, badala yake, nitapata laana,
Siyo hadharani, ila itakolea moyoni,
Kilemba cha ukoka, sifa za kujipendekeza,
Zisizo za moyoni, bali zatokana na woga.
Seyton!

**Seyton** *Anaingia.*

SEYTON: Wahitaji nini, mtukufu?
MAKBETH: Kuna habari gani mpya?
SEYTON: Mfalme wangu, taarifa uliyoletewa
Imethibitika.
MAKBETH: Nitapigana hadi mwili wangu ukatwekatwe,
Ubaki mifupa mitupu. Nipe deraya yangu.
SEYTON: Haijahitajika bado.
MAKBETH: Nitaivaa.
Wapeleke madoria zaidi wenye farasi,
Wapite mbio na kupeleleza nchi nzima;
Nyonga wote wanaozungumza juu ya woga.
Nipe deraya yangu.
Yule mgonjwa ana hali gani sasa, daktari?
DAKTARI: Cha mno si ugonjwa, habibi wangu,
Kwani kimtesacho akilini ni jinamizi,
Ambalo humnyima usingizi na utulivu.
MAKBETH: Mponye maradhi hayo:
Je, huwezi kuutibu ubongo wenye maradhi,
Usafishe huzuni iliyokolea moyoni,
Ubandue taabu zilizonata ubongoni,
Na kwa msaada wa dawa tamu ya usingizi,
Usafishe kifua kilichojaa farafara,
Mambo ya hatari yenye kulemea moyo wake?
DAKTARI: Katika maradhi ya jinsi hii
Yamlazimu mwele kuitibu nafsi yake.
MAKBETH: Wape mbwa uganga wako; sina haja nao tena.
Haya njoo, Seyton, nivike deraya yangu;
Nipe kirungu changu: tuma madoria zaidi.
Naam, daktari, masheki wangu waniacha.
Haya, Seyton, fanya haraka. Ah, daktari,

Laiti ungeweza kuuyakinisha ugonjwa
Wa milki yangu hii, na halafu kuiponya,
Irudiwe na afya yake ya mwanzo; hakika,
Ningalikusifu kwa shangwe na vifijo mpaka
Mwangwi wa sauti yangu ukariri sifa hizo.

(*kwa Seyton*)

Nivike deraya hii; sikia ninavyosema.—

(*kwa Daktari*)

Miti-shamba gani, sanamaki, au dawa gani,
Iwezayo kuwafukuza hawa Waingereza?
Umesikia habari ya kuja kwao?

DAKTARI: Naam, bwana adilifu; matayarisho yako
Ya kivita yametupa fununu ya kuja kwao.

MAKBETH: (*kwa Seyton*): Nifuate na deraya hiyo.
Sitaogopa wala kifo wala maangamizi,
Hadi msitu Benamu ufike Dansinane.

DAKTARI (*kando*): Laiti ningaliweza kuhama Dansinane,
Tamaa ya mali isingeweza kunirudisha.

(*Wanaondoka.*)

**Onyesho la 4. Mbugani, karibu na msitu wa Benamu.** *Ngoma na beramu. Wanaingia* **Malkom, Mzee Siwadi,** *na mwanawe,* **Makdaff, Menteth, Kathne, Angasi, Lenoksi, Ross,** *na Askari wakiwa katika mwendo.*

MALKOM: Binamu zangu, natumai siku zakaribia,
Ambazo tutaishi makwetu kwa usalama.

MENTETH: Hatuna mashaka.

SIWADI: Msitu ulio mbele yetu waitwaje?

MENTETH: Msitu wa Benamu.

MALKOM: Kila askari ajikatie tawi la mti,
Ajifunike upande wa mbele; kwa njia hiyo,
Madoria watashindwa kujua idadi yetu,
Wapeleke taarifa isiyo ya kweli.

ASKARI: Hilo litatendeka.

SIWADI: Tumesikia hamna mwingine ila beberu
Anayejiamini katulia Dansinane,
Na atarajia kutupinga tukimzingia.

MALKOM: Hilo ndilo tumaini lake kubwa:
Kwani wasaa ufaao unapojitokeza,
Wakubwa kwa wadogo wameasi amri yake,
Ye yote anayemtumikia kalazimishwa,
Na huduma jinsi hiyo haitoki moyoni.

MAKDAFF: Tusiwe na matumaini yapitayo kiasi,
Tungoje matokeo yaudhihirishe ukweli
Wa dhana zetu, ila kwa sasa tujitayarishe,
Tuwe askari walio hodari.

SIWADI: Wakati wakaribia,
Ambapo tutaweza kuwa na hakika kabisa
Ya mambo tuliyopoteza na tuliyofaidi,
Mawazo yetu kwa sasa ni ya kubahatisha tu,
Twajivika tumaini bila kujua ukweli,
Lakini uamuzi utafanywa na mapigano:
Hivyo tufunge safari kuelekea vitani.

(*Wanaondoka kwa gwaride.*)

## Onyesho la 5. Dansinane. Ndani ya ngome.

*Wanaingia* **Makbeth, Seyton,** *na Askari wakiwa na ngoma na bendera.*

MAKBETH: Tutundike bendera zetu katika kuta za nje;
Sikuzote watu hulia kwa woga, 'Wanakuja:'
Ngome yetu ina nguvu kudhihaki mazingiwa:
Washinde hapa mpaka wafe kwa njaa na homa:
Kama idadi yao haikuongezwa na wale
Ambao walistahili kuwa upande wetu,
Tungewakabili kikakamavu uso kwa uso,
Na kuwatandika hata wakimbilie makwao.

(*Kilio cha wanawake ndani.*)

Kelele gani hizo?

SEYTON: Ni makelele ya wanawake, bwana wangu mwema

(*Anaondoka.*)

MAKBETH: Sasa ni karibu niusahau woga kabisa:
Kumepata kuwa wakati, ambao damu yangu
Ingegandishwa na woga kwa kilio cha usiku;
Na kama nilisikia hekaya inayotisha,
Nywele zilisimama wimawima kichwani mwangu,

Zikajitikisatikisa kama zenye uhai:
Sasa vitisho vimekwisha kuwa ni kawaida;
Mawazo ya kiuaji yamezoea msiba,
Ambao hauwezi tena kunitisha.

**Seyton** *anarudi.*

Kilio hicho kilikuwa cha nini?

SEYTON: Bwana wangu Malkia amekufa.

MAKBETH: Sharti angekufa wakati fulani ujao;
Taarifa ya kifo chake budi ingesikilika.
Kesho, na kesho, kisha kesho, hufuatana hivyo,
Katika utaratibu wa upuzi kila siku,
Hadi kufikia silabi ya mwisho ya maisha;
Na jana zetu zote zimewaonyesha wajinga
Njia ya kifo, kuirudia hali ya udongo.
Basi zimika, ewe mshumaa usiyedumu!
Maisha ni mfano wa kivuli kitembeacho,
Mchezaji maskini anayejifaharisha
Kwa muda mfupi katika dungu la ulimwengu,
Kisha akatoweka wala asisikike tena:
Ni hadithi inayohadithiwa na anzali,
Yenye kelele na ghadhabu, isiyo na maana.

*anaingia Mjumbe.*

Waleta habari fulani; haya sema upesi.

MJUMBE: Bwana wangu mtukufu,
Yapasa nitoe taarifa ya nilichoona,
Lakini sijui jinsi gani nitakisema.

MAKBETH: Haya, sema, bwana.

MJUMBE: Niliposimama juu ya mlima nikichunga,
Nilitazama upande wa msitu wa Benamu,
Mara niliona kama kwamba msitu huo
Ulianza kusogea.

MAKBETH: U mwongo na kitwana!

MJUMBE: Nitavumilia adhabu, kama ninaongopa:
Umbali wa maili tatu waweza kuona,
Nasema, ni miti inayotembea.

MAKBETH: Kama waongopa sharti unyongwe kwenye mti
Ulio karibu kuliko yote ukiwa hai,
Mpaka njaa ikufanye ukunjamane kau:
Walakini kama taarifa yako ni ya kweli,

Sitajali kama wewe ukinitendea vivyo.
Ninapinga mambo anayosema, lakini sasa
Naanza kuwatilia shaka wale wachawi,
Wanaoongopa chini ya kivuli cha ukweli:
"Kamwe usiogope, mpaka msitu Benamu
Ujiondoshe ukielekea Dansinane."
Na sasa msitu wakaribia Dansinane.
Jienezeni silaha, hima twendeni vitani!
Kama kweli hicho anachosema kinatokea,
Hamna kimbilio, na siwezi kubaki hapa.
Sasa mwanga wa maisha waanza kunichosha,
Na heri mambo yote duniani yarabishike.
Piga kamsa! Upepo, vuma! Njoo, ma'ngamizi!

## Onyesho la 6. Dansinane. Mbele ya ngome.

*Ngoma na bendera. Wanaingia* **Malkom,** *Mzee* **Siwadi, Makdaff** *na Jeshi, wakibeba matawi.*

MALKOM: Sasa tumefika karibu ya kutosha; tupeni
Matawi yenu chini; mj'onyeshe mlivyo hasa.
Wewe, mjomba mheshimiwa, na binamu yangu,
Aliye mwanao mtukufu, mtakiongoza
Kikosi cha kwanza: mheshimiwa Makdaff,
Na sisi tutakamilisha yatakayobakia,
Kwa mwujibu wa mpango wetu maalum.

SIWADI: Buriani.
Na laiti tungepambana na jeshi la beberu
Usiku wa leo, watushinde kama hatuwezi
Kupigana.

MAKDAFF: Pigeni matarumbeta yetu yasikike pote;
Yapeni pumzi zote; yawe ni matangulizi
Ya hoihoi ya umwagaji wa damu na kifo.

(*Wanaondoka.*)

## Onyesho la 7. Sehemu nyingine ya mbuga.

*Kamsa. Anaingia* **Makbeth.**

MAKBETH: Wamenizunguka pote: siwezi kuwakimbia,
Bali, kama dubu anowindwa, nitajitetea.

Mtu gani huyo asozaliwa na mwanamke?
Yapasa nimwogope mtu wa jinsi hiyo tu,
La sivyo, sitamwogopa ye yote.

*Anaingia* **Siwadi** *Mdogo.*

SIWADI MDOGO: Jina lako nani?
MAKBETH: Utatishika ukilisikia.
SIWADI MDOGO: La; hata ungalijiita jina linalotisha
Kuliko jina lo lote la jehanamu.
MAKBETH: Jina langu ni Makbeth.
SIWADI MDOGO: Ibilisi halisi hangeweza kutaja jina
Linalochukiza sikio langu kama hilo.
MAKBETH: Hapana, wala linalotisha zaidi ya hilo.
SIWADI MDOGO: Waongopa, beberu makuruhi; kwa sime yangu
Nitaudhihirisha uongo unaotamka.

(*Wanapigana, na Siwadi Mdogo anauawa.*)

MAKBETH: Wewe ulizaliwa na mwanamke.
Ila mimi nadharau sime, nabeza silaha
Zinazopungwa na alozaliwa na mwanamke.

(*Anatoka.*)

*Kamsa. Anaingia* **Makdaff.**

MAKDAFF: Kelele zatoka huko. Beberu, j'onyeshe uso!
Kama umechinjwa na mwingine bila pigo langu,
Mizuka ya mke na wanangu itanisumbua.
Siwezi kupigana na vijiaskari duni,
Ambavyo vimeajiriwa kubeba mikuki tu:
Au nipambane nawe binafsi, Makbeth,
Au la, sime yangu, bila ncha yake kuguswa,
Niirudishe alani bila kutenda cho chote.
Sharti uwe mahali hapo; kwa kelele hizo,
Najua kuna kabaila anayeshangiliwa.
Nimwone, bahati! Siombi majaliwa zaidi.

(*Anaondoka. Kamsa.*)

*Wanaingia* **Malkom** *na* **Mzee Siwadi.**

SIWADI: Njoo huku, bwana wangu; ngome imejitolea
Bila upinzani: na askari wa beberu
Wapigana pande mbili, upande wake na wetu;

Masheki adhimu watupigania kishujaa;
Ni karibu siku yenyewe ijitangaze yako,
Na si mengi yamebaki kukamilisha ushindi.

MALKOM: Tumekuta mahasimu wanaotupigania.

SIWADI: Ingia, bwana, kwenye ngome.

(*Wanaondoka. Kamsa.*)

**Onyesho la 8.** Sehemu nyingine ya **mbuga.**

*Anaingia* **Makbeth.**

MAKBETH: Kwa nini niige mchezo wa Mrumi mjinga,
Kujiua kwa sime yangu? Iwapo ninaona
Mahasimu waishi, heri kuwajeruhi wao.

*Anaingia* **Makdaff.**

MAKDAFF: Nigeukie, fidhuli wa jehanamu geuka!

MAKBETH: Miongoni mwa watu wote nimekwepuka wewe:
Lakini rudi ulikotoka; kwani roho yangu
Imejaa farafara damu ya ahali zako.

MAKDAFF: Mimi sina maneno:
Sauti yangu dhihirifu katika sime yangu;
Wewe mwuaji nduli nisivyoweza kueleza!

(*Wanapigana.*)

MAKBETH: Unajisumbua bure:
Kuijeruhi hewa isiyotilika jeraha,
Ni rahisi kama kunifanya nitokwe na damu:
Angusha simeyo juu ya vichwa vishindikavyo;
Nina maisha yaliyokagwa, yasiyoshindika
Na awaye yote alozaliwa na mwanamke.

MAKDAFF: Usitegemee uramali wako;
Na malaika ulomtumikia siku zote
Akwambie, Makdaff alitoka kwenye tumbo
La mama la uzazi kabla ya mimba pevu.

MAKBETH: Maluuni na ulimi unaoniambia hayo,
Kwani 'metiisha sehemu bora za utu wangu!
Na mazimwi ya vipengee yas'aminike tena,
Wanaofumbia mafumbo yenye maana mbili;
Wanotuwekea neno la ahadi sikioni,
Na kughairi, kuharibu matumaini yetu.
Sitapigana nawe.

MAKDAFF: Basi na ujitoe, mwoga,
Na uishi kama kionyesho cha wakati huu:
Tutafurahiwa kuwa nawe, kama tupendavyo
Kuwa na nduli wanaopatikana kwa nadra,
Uchorwe juu ya kitambaa kilichoandikwa,
'Hapa unaweza kumwona yule beberu.'

MAKBETH: Siwezi kujitoa,
Niibusu ardhi ipakanayo na miguu
Ya kijana Malkom; na akina yahe nao
Wanitupie matusi ya laana: hata kama
Msitu wa Benamu umekuja Dansinane,
Na kweli ya kuwa hukuzaliwa na mwanamke,
Bado nitajitahidi mpaka nione mwisho.
Mbele yangu najikinga kwa ngao yangu ya vita:
Choma Makdaff, ukiweza, na alaaniwe
Yule atayeanza kulia 'Acha, yatosha!'

(*Wanatoka wakipigana. Kamsa.*)

(*Mdundo wa marejeo. Wanaingia na ngoma na bendera:* **Malkom,** *Mzee* **Siwadi, Ross,** *wale Masheki wengine, na Askari.*

MALKOM: Laiti wenzetu wanaokosekana hapa
Wangefika kwa usalama.

SIWADI: Baadhi yao ni sharti wafe; na hata hivyo,
Kwa idadi ninayoona hapa budi niseme,
Ushindi mkubwa hivyo 'megharimu bei ndogo.

MALKOM: Makdaff hayupo, pia mwanao mtukufu.

ROSS: Mwanao, bwanangu, kalipa deni la askari:
Kadiriki kuishi kufikia utu uzima;
Na baada ya kudhihirisha uhodari wake,
Katika mapigano ambayo hayakumtisha,
Alikufa kiume.

SIWADI: Basi amekufa?

ROSS: Ndiyo, na katolewa nje ya mgunda wa vita:
Huzuni yako isipimwe na utukufu wake,
Kwani, kuipima hivyo, haiwezi kupimika.

SIWADI: Kapata majeraha upande wa mbele wa mwili?

ROSS: Naam, katika paji la uso.

SIWADI: Basi, kawa askari kwenye huduma ya Mungu!
Ningalikuwa na wana wengi kama nywele zangu,
Nisingewatakia kifo chema kuliko hicho:

Na hivyo, kengele ya mauti yake imepigwa.
MALKOM: Anastahili majuto mengi kuliko hayo,
Nitatafuta wasaa n'omboleze ipasavyo.
SIWADI: Hastahili zaidi:
Wamesema kafa kiume, akalipa deni
Limpasalo kila askari: kwa hiyo,
Mungu ampe malazi mema! Ninatumaini
Habari mpya inayokuja yaleta faraja.

*Anaingia* **Makdaff,** *akichukua kichwa cha* **Makbeth.**

MAKDAFF: Salamu mfalme! kwani hicho ni cheo chako:
Tazama mahali kilipo kichwa chenye laana,
Cha beberu aliyekumba mamlaka kwa nguvu:
Taifa letu sasa liko huru: ninakuona
Wazungukwa na waheshimiwa wa milki yako,
Wanokusalimu pamoja nami myoni mwao;
Ambao nawasihi waiunge sauti yangu:
Salamu, Mfalme wa Skotia!
WOTE: Salamu, mfalme wa Skotia!

(*Matarumbeta.*)

MALKOM: Sitapoteza wakati mwingi bila kumtuza
Kila mmoja wenu kwa huduma ya mapenzi,
Ili niwalipe thawabu mnayostahili.
Masheki na ahali, sasa kuweni masharifu,
Kilicho cheo kipya kabisa hapa Skotia,
Katika shangwe la ushindi mkubwa kama huu.
Jambo jingine, ambalo sharti litendwe hima,
Ni kuwaita ndugu waliokimbilia ng'ambo,
Na kisha tuwasake wale wajumbe wakatili,
Wa huyu mwuaji mfu na malkia shetani,
Ambaye, kama idhaniwavyo, kwa mikono yake,
Kajiondolea uhai wake; hayo, pamoja
Na yatakayotupasa, kwa msaada wa Mungu,
Tutayatenda mara wasaa ukijitokeza:
Kwa hiyo nashukuru wote, na isimu ya mtu,
Ambao tunawaalika mje huko Skone,
Kwenye sherehe za kutawazwa.

(*Matarumbeta. Wanaondoka.*)

TAMATI

# KAMUSI FUPI

## A

**Adilifu:** —enye heshima, haki na wema.
**Afkani:** mtu mwenye akili pungufu.
**Aghalabu:** mara nyingi, zaidi, hasa.
**Agia:** kuahidi.
**Agua:** kuonya juu ya mambo yatakayotokea, kubashiri.
**Ahali:** mke au jamaa, ndugu.
**Akraba:** ndugu, jamaa, ahali.
**Amali:** kitendo, kazi, mazoea.
**Ambaa:** kujitenga na kitu au mtu, kuwa mbali na.
**Ambata:** kushikamana, kunata.
**Anzali:** mtu dufu na mjinga kupindukia, msungo.
**Ashekali:** nafuu katika ugonjwa au maumivu.
**Athari:** waa, kasoro, alama.
**Atuka:** kupasuka.

## B

**Baathiwa:** siku ya kubaathiwa ni siku ya kufufuliwa wafu; siku ya kiyama.
**Bellona:** (Kilatini) muungu wa kike wa vita.
**Beza:** kudharau.
**Buriani:** maagano, kwa heri.
**Buruji:** ngome, boma lenye kuta zenye mapengo kwa juu.
**Bwabwaja:** kuzungumza bila maana, kupayapaya.

## C

**Changamana:** kuwa katika hali ya kuchanganyika.

## D

**Deraya:** kisibau cha chuma cha kivita.
**Dhana:** wazo, maono.
**Dhihaki:** kufanya mzaha.
**Dhurika:** kuumizwa, kuhasirishwa.
**Diriki:** kuweza, kuwahi au kupata yaliyokusudiwa.
**Dohani:** bomba la kutolea moshi.
**Doria:** askari wapelelezi.
**Dubu:** namna moja ya mnyama wa mwituni.
**Dufu:** hafifu, isiyofaa. [Mara dufu ni mara mbili.]
**Dungu:** [Jukwaa,] kilingo.
**Duwaa:** kushikwa na bumbuazi, kushangaa.

## E

**Elemeza:** kufunikiza kabisa, kushinda kabisa.

F

**Fadhili:** upendo, ukarimu, hisani.
**Fafanua:** kueleza, kufanya wazi, kufahamisha.
**Farafara:** kujaza kitu au chombo farafara ni kukijaza mpaka ukingoni.
**Fauwa:** mamoja, sawasawa.
**Feli:** kufumania, kugundua mabaya au mambo ya siri.
**Fichua:** kinyume cha kuficha.
**Fifisha:** kupoteza nguvu au uzuri wa kitu.
**Fuadi:** moyo.
**Fumbata:** kushika mkononi, kuzungushia mikono.
**Fyata:** kufyata ulimi ni kunyamaza kimya.

G

**Ghairi:** kubadili nia, kuacha jambo lililokusudiwa kwanza.
**Ghamu:** taabu au majonzi.
**Ghulamu:** kijana mwanamume.
**Gubigubi:** kabisa. kujifunika gubigubi ni kujifunika kabisa.

H

**Habibi:** bwana, hababi, jina la heshima.
**Habithi:** mtu mwenye ukatili.
**Hadaiwa:** kudanganywa.
**Hadhi:** [staha,] heshima, cheo.
**Haini:** mtu asiyeaminika, mdanganyi.
**Hamanika:** kuhangaika, kuona wasiwasi.
**Hanamu:** mshazari, kombo.
**Harara:** joto, hari, haraka na nia ya kutenda jambo.
**Hasimu:** adui, mtesi.
**Hatima:** mwisho, kikomo.
**Hayawani:** mnyama, mtu mwenye tabia na hali ya kinyama.
**Hekaya:** hadithi, kisa, jambo la ajabu.
**Hisa:** sehemu, fungu, mgao.
**Hobelahobela:** bila taratibu.
**Hoihoi:** zahama, ghasia n.k.
**Huduma:** utumishi, matendo ya fadhili.
**Huisha:** kufufua, kutia uhai au uzima.

I

**Ijara:** mshahara, fedha za utumishi.

J

**Jabari:** mtawala mkuu wa pekee; hodari, shujaa.
**Jahili:** mtu atendaye mambo bila hofu, [mtu katili.]
**Jazi:** kupa, kupa thawabu; kulipa kwa kitendo chema.
**Jedwali:** orodha.

**Jidhili:** kujishusha.
**Jigamba:** kujisifu, kujivuna, kujiona.
**Jilisi:** kukaa na kuzungumza.
**Jinamizi:** ndoto ya kutisha.
**Jinaya:** Jinai, taksiri, kesi kubwa.
**Jipapatushe:** jiepushe na, tupilia mbali, ambaa na kitu.
**Jiri:** kutokea, kutukia.
**Jirudi:** kujigombeza mwenyewe kwa majuto.
**Jitimai:** sikitiko, huzuni, majonzi.

K

**Kabaila:** mtu wa ukoo bora.
**Kaga:** kulinda kwa uganga, talasimu au hirizi.
**Kamsa:** tarumbeta, kengele ya kujulisha hatari, kelele.
**Kasisi:** Padre.
**Kefule:** neno la kuonyesha mshangao au chuki.
**Kero:** ghasia, masumbuko, uchokozi, udhia.
**Kibeti:** mbilikimo, mtu mdogo kuliko kawaida.
**Kibuhuti:** majonzi, hofu ya mambo yajayo.
**Kiherehere:** kipigopigo cha moyo, hofu, wasiwasi.
**Kilalio:** chakula cha jioni.
**Kilinge:** baraza, mahali pa watu kukutana.
**Kimbimbi:** nywele zilizosimama wima kwa sababu ya baridi au hofu nyingi.
**Kimbunga:** tufani, dhoruba, upepo wenye nguvu nyingi.
**Kinaganaga:** waziwazi.
**Kinundu:** nundu ndogo, sehemu iliyotokeza.
**Kiolezo:** mfano wa kufuatwa.
**Kipanga:** namna ya ndege mkubwa anayekula wanyama wadogo.
**Kipupwe:** majira ya baridi.
**Kirihifu:**—enye kuchukiza.
**Kitwea:** upweke, hali ya kukaa mahali pa pekee.
**Kodoa:** kutazama kwa macho yaliyokazwa, kutoa macho.
**Kukurika:** kushughulika sana.
**Kumba:** twaa kwa choyo, chukua vitu au mali kwa choyo.
**Kupindukia:** kabisa, mno.

L

**Lemeza:** kulemea kabisa, kuzidia, kuzidi nguvu na kushinda.
**Limatia:** kawia, chelewa.
**Liwaza:** tuliza, sahaulisha, tumbuiza.
**Lukuki:** hesabu kubwa isiyohesabika.

M

**Maadili:** mambo mema, mambo ya haki, mambo yapendezayo.
**Majaliwa:** msaada, rehema, neema, thawabu.
**Makuruhi:** karaha, machukizo.
**Maluuni:** shetani, aliyelaaniwa.

**Manga:** Uarabu, Arabuni, Bara Arabu.
**Marigedi:** sufuria kubwa.
**Masimbi:** mashudu; taka zilizosalia baada ya kuchuja kitu.
**Matao:** mapindi, makunjo, kombo.
**Matimtimu:** ovyo ovyo; nywele za matimtimu ni nywele zisizosukwa wala kulazwa vizuri.
**Mavilio:** mavilio ya damu ni damu iliyoganda.
**Maumbile:** sura, umbo, tabia.
**Mbari:** kabila, ukoo.
**Minajili:** kwa ajili ya.
**Mitutu:** mtutu wa bunduki ni mwanzi wake; kasiba.
**Mkirimu:** mkaribishaji; mwenye kufanya ukarimu kwa wageni.
**Mlaghai:** ayari, mbazazi, mwenye kudanganya kwa maneno.
**Mpayupayu:** mwenye kupayuka, mwenye kusema maneno ya upuzi.
**Mshaufu:** mpujufu; mtu asiye na haya wala adabu.
**Msoa:** kundi la watu, hasa katika safari, wafuasi, msururu.
**Mstahiki:** mtu anayestahili heshima na kuwekewa adabu.
**Mumiani:** namna ya dawa.
**Murua:**—zuri, —a kupendeza, —a maana.
**Mwanasesere:** bandia wa mtoto.
**Mwele:** mgojwa.
**Mwenzi:** rafiki.
**Mzandiki:** mnafiki, mwongo, mdanganyi.
**Mzuka:** pepo, zimwi, mtu atokeayé ghafula.

N

**Nasaba:** jadi, asili.
**Nawiri:** kung'aa sana
**Nduli:** dhalimu, katili, n.k.
**Neptune:** (Kilatini) muungu wa bahari.
**Nufaisha:** kufaa, kufaidi.
**Nuksani:** nuksi, mkosi, ugomvi, waa.
**Nyatia:** nyemelea.
**Nyenje:** mdudu kama panzi.
**Nywea:** kukonda, kujikunja.

O

**Ongopa:** kusema uongo.
**Otea:** kuvizia, kujificha kwa madhumuni ya mashambulio.

R

**Rabishika:** kuwa katika hali ya fujofujo, wasiwasi n.k.
**Rabsha:** kelele, ghasia, ugomvi.
**Reale:** sarafu iliyokuwa na thamani ya shilingi 2/85.
**Rekebisha:** kusahihisha, kuweka sawa.
**Ridhia:** kukubali, kukubalia, kupendezwa na, kuidhini.
**Rishai:** kupapa, kuloa, kuwa na majimaji.

S

**Sadifu:** kutokea barabara ilivyosemwa au ilivyotazamiwa.

**Safihi:** fidhuli, jeuri.
**Safii:** safihi.
**Saisi:** mtumishi mwenye kazi ya kutunza punda au farasi.
**Sakini:** kukaa mahali, kufanya makao.
**Salimika:** kuokoka, kunusurika, kutoka hatarini.
**Selea:** kusalia au kubakia na kukaa mahali kabisa au kwa muda mrefu.
**Shabihiana:** kushabihi, kufanana na, kuwa sawasawa na.
**Shaghala baghala:** shelabela; ovyo ovyo, bila utaratibu.
**Shani:** jambo la ajabu au la kushangaza.
**Shari:** uovu, msiba, chuki, bahati mbaya, ugomvi.
**Sharifu:** —enye [sifa,] heshima, na utukufu.
**Shariti:** kushariti maneno ni kusema uwongo.
**Sheki:** sheik, mzee mheshimiwa, mtu mwenye cheo kikubwa.
**Shutumu:** kutukana, kulaumu, kukemea, kusingizia.
**Sibu:** kutukia, kutokea.
**Sononeka:** kuumia, kuona maumivu, kusumbuka.
**Sufii:** mtawa, mcha Mungu, walii.

T

**Tafakari:** kufikiri, kuwaza.
**Tahayari:** kufedheheka, kuaibika, kuona soni, kuwa na haya.
**Takwimu:** orodha ya siku za mwaka, kalenda.
**Taswira:** picha, sanamu, sura, mfano, mithali.
**Tawasufi:** kiasi katika mambo.
**Tawaza:** kutawalisha, kummikilisha mtu.
**Tetesi:** mnong'ono wa habari, uvumi.
**Teule:** iliyochaguliwa, au kuteuliwa.
**Tiisha:** kushinda, kufanya kutii.
**Titimka:** timka, kwenda mbio au kwa ghafula.
**Tufe:** kitu cha mviringo kama chungu au mpira.
**Tunu:** Kitu cha thamani, hedaya, zawadi.
**Tusitusi:** —enye gizagiza, —eusi.

U

**Ubapa:** uso wa kitu ulio sawasawa k.m. ubapa wa panga.
**Ucheshi:** uchekeshaji, hali ya kuchekesha na kufurahisha.
**Ufanisi:** usitawi, maendeleo mema.
**Ujuvi:** ufidhuli, utundu, kiburi.
**Unyofu:** upole, haki, uadilifu.
**Uramali:** uchawi wa kupelekwa, si wa kulishwa, ulozi.
**Usihiri:** uchawi, ulozi, hirizi.
**Uzushi:** tendo au mambo ya kuvumbua; tukio la ghafula.

V

**Vigaga:** vipande vya damu au usaha vilivyoganda juu ya kidonda au jeraha.
**Vipengee:** maneno yenye vipengee ni maneno yenye hila na ambayo yamekusudiwa kumzungusha mtu.

W

**Wakf:** kilichowekwa kwa matumizi maalum ya kipekee, au kwa matumizi ya dini au ibada.

Y

**Yakinisha:** kuhakikisha, kuthibitisha.
**Yamini:** kiapo.
**Yumkini:** yamkini, huenda ikawa.

Z

**Zaka:** sadaka.
**Zawaridi:** namna moja ya ndege.
**Zinduka:** kuamka ghafula katika usingizi.
**Zingia:** kuuzunguka mji vitani; kuzingira; kufanya mazingiwa.
**Zua:** kuvumbua; kubuni habari zisizo za kweli.